Sudan Kusini

Kitabu cha mwanafunzi

# Kiswahili 2

**Kiswahili kwa kidato cha pili(2)** kimeandikwa na wizara ya Elimu na Mafunzo kwa jumla, Ikishirikiana na wataalam wa lugha.

Kitabu hiki kinamwelimisha mwanafunzi kwa mazoezi na vitendo.

**Kila darasa linajumuisha Kitabu cha Mwanafunzi na Mwongozo wa Mwalimu.**

**Kila Kitabu cha mwanafunzi kinakupa:**

- Ufafanuzi mwafaka wa mtaala wa kitaifa.
- Msingi bora katika kiswahili.
- Uwasilishaji na ufafanuzi wa hoja unazotakiwa kujifunza.
- Mazoezi mwafaka yanayoonyesha jinsi Kiswahili Kinaweza kutumika katika mifano halisi maishani.
- Fursa ya ushirikiano kupitia kwa kazi ya vikundi.
- Michoro ya kusisimua.

**Masomo yote katika mfululizo huu wa msingi yalitengenezwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Mkuu, Jamhuri ya Sudan Kusini.**

**Vitabu vimeundwa kutekeleza somo la shule za msingi,na wakati huo huo kuwawezesha wanafunzi na ujuzi unaofaa katika jamii ya kisasa ya kimataifa**

**Kitabu hiki ni Mali ya Wizara ya Elimu na Mafunzo.**

**Kitabu hiki hakiruhusiwi kuuzwa.**

**Kitabu kitakachopatikana kikiuzwa kwa njia yoyote kitatawaliwa na muuzaji kuchukuliwa hatua za kisheria.**

**Kimefadhiliwa na:**

GLOBAL PARTNERSHIP for EDUCATION
quality education for all children

Sudan Kusini

THE REPUBLIC OF SOUTH SUDAN
MINISTRY OF GENERAL EDUCATION AND INSTRUCTION

Kitabu cha mwanafunzi

# Kiswahili 2

## Kidato cha Pili



**Kitabu hiki ni Mali ya Wizara ya Elimu na Mafunzo.**

**Kitabu hiki hakiruhusiwi kuuzwa.**

**Kimefadhiliwa na:**

GLOBAL PARTNERSHIP for EDUCATION
quality education for all children

# Jinsi ya kutunza kitabu chako.

**Mambo muhimu ya kuzingatia**

1. Unaombwa kuhakikisha umenawa mikono kabla ya kukitumia kitabu chako.
2. Tumia kalamu ya rangi kuonyesha kazi iliyofanywa.Usikunje karatasi za vitabu.
3. Kitabu kikiharibika,hakikisha kinakarabatiwa kwa haraka.
4. Kuwa mwangalifu wakati unapomwazimu mwenzako kitabu.
5. Tafadhali kiweke kitabu chako mahali pakavu na pasipokuwa na unyevu.
6. Unapokipoteza kitabu chako, mjulishe mwalimu wako.

**Mambo unayokatazwa kufanya.**

1. Usiandike ndani au juu ya kitabu chako.
2. Usikate michoro iliyokitabuni.
3. Usirarue kurasa zozote kitabuni.
4. Usikiache kitabu kikiwa kimefunguliwa.
5. Usikiweke kitabu chako kwenye mkoba uliojazwa vitabu zaidi.
6. Usikitumie kitabu chako kujifunika wakati wa mvua.
7. Usikikalie kitabu chako.

Sudan Kusini

KIDATO CHA
2

# Kiswahili

*Kitabu cha Mwanafunzi*

© 2018, THE REPUBLIC OF SOUTH SUDAN, MINISTRY OF GENERAL EDUCATION AND INSTRUCTION.
All rights reserved. No part of this book may be reproduced by any means graphic, electronic, mechanical, photocopying, taping, storage and retrieval system without prior written permission of the Copyright Holder.Pictures, illustrations and links to third party websites are provided in good faith, for information and education purposes only

Kitabu hiki ni Mali ya Wizara
Kimetadhiliwa na: ya Elimu na Mafunzo.

Ilifadhiliwa na:
GLOBAL PARTNERSHIP for EDUCATION
quality education for all children

**KITABU HIKI HAKIRUHUSIWI KUUZWA.**


FOREWORD

I am delighted to present to you this textbook, which is developed by the Ministry of General Education and Instruction based on the new South Sudan National Curriculum. The National Curriculum is a learner-centered curriculum that aims to meet the needs and aspirations of the new nation. In particular, it aims to develop (a) Good citizens; (b) successful lifelong learners; (c) creative, active and productive individuals; and (d) Environmentally responsible members of our society. This textbook, like many others, has been designed to contribute to achievement of these noble aims. It has been revised thoroughly by our Subject Panels, is deemed to be fit for the purpose and has been recommended to me for approval. Therefore, I hereby grant my approval. This textbook shall be used to facilitate learning for learners in all schools of the Republic of South Sudan, except international schools, with effect from 4th February, 2019.

I am deeply grateful to the staff of the Ministry of General Education and Instruction, especially Mr Michael Lopuke Lotyam Longolio, the Undersecretary of the Ministry, the staff of the Curriculum Development Centre, under the supervision of Mr Omot Okony Olok, the Director General for Quality Assurance and Standards, the Subject Panelists, the Curriculum Foundation (UK), under the able leadership of Dr Brian Male, for providing professional guidance throughout the process of the development of National Curriculum and school textbooks for the Republic of South Sudan since 2013. I wish to thank UNICEF South Sudan for managing the project funded by the Global Partnership in Education so well and funding the development of the National Curriculum and the new textbooks. I am equally grateful for the support provided by Mr Tony Calderbank, the former Country Director of the British Council, South Sudan; Sir Richard Arden, Senior Education Advisor of DfID, South Sudan. I thank Longhorn and Mountain Top publishers in Kenya for working closely with the Ministry, the Subject Panels, UNICEF and the Curriculum Foundation UK to write the new textbooks. Finally, I thank the former Ministers of Education, Hon. Joseph Ukel Abango and Hon. Dr John Gai Nyuot Yoh, for supporting me, in my previous role as the Undersecretary of the Ministry, to lead the Technical Committee to develop and complete the consultations on the new National Curriculum Framework by 29 November 2013.

The Ministry of General Education and Instruction, Republic of South Sudan, is most grateful to all these key stakeholders for their overwhelming support to the design and development of this historic South Sudan National Curriculum. This historic reform in South Sudan's education system is intended to benefit the people of South Sudan, especially the children and youth and the future generations. It shall enhance the quality of education in the country to promote peace, justice, liberty and prosperity for all. I urge all Teachers to put this textbook to good use.

May God bless South Sudan. May He help our Teachers to inspire, educate and transform the lives of all the children and youth of South Sudan.



Deng Deng Hoc Yai, (Hon.)

**Minister of General Education and Instruction, Republic of South Sudan**

# YALIYOMO


SURA YA 1 Mada kuu: MAAMKUZI ............................................ 1

SURA YA 2 Mada kuu: UHIFADHI WA MAZINGIRA................ 10

SURA YA 3 Mada Kuu: UHIFADHI WA ................................... 18

SURA YA 4 Mada kuu: UNUNUZI NA UUZAJI WA BIDHAA... 29

SURA YA 5 Mada kuu: AFYA NA MAGONJWA ......................... 58

SURA YA 6 Mada kuu: MILA, UTAMADUNI NA ITIKADI .... 72

**SURA YA 1**

# Mada kuu: MAAMKUZI

**Mada Ndogo ya 1:** **Kusikiliza na kuzungumza**

## Maamkuzi

| | |
|---|---|
|  |  |

Maamkuzi ni njia ya kusalimiana na kujuliana hali. Kitendo cha salamu hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Baadhi ya watu husalimiana kwa mikono,wengine hupiga magoti,hushikwa utosini na utamaduni wa wengine hauwaruhusu kusaliamiana kwa mkono. Kuna maamkuzi ya asubuhi,mchana na wakati wowote.

## Soma maamkuzi yafuatayo na wakati wake.

| wakati | salamu | jibu |
|---|---|---|
| Asubuhi | Sabalheri | Sabalheri/Aheri/Alkheri! |
| jioni | Masalheri | Masalheri/Aheri/Alkheri! |
| usiku | Alamsiki! | Binuru! |
| Wakati wowote | Hujambo | Sijambo! |
| | Shikamoo | Marahaba! |
| | Salaam aleikum! | Aleikum salaam! |
| | Uhali gani? | Njema! |

**Maamkuzi huandamana na maneno ya adabu. Haya ni maneno yanayoonyesha adabu na heshima.Soma.**

| | |
|---|---|
| 1.Asante | Hutumiwa kuonyesha shukrani. |
| 2.Pole | Nineno mtu aliyefikwa na jambo kama vile kifo au ajali ili kumfariji. |
| 3.Samahani | Ni neno la kuomba ruhusa ya kutenda jambo fulani au kuomba radhi. |
| 4.Tafadhali | Ni neno la kumuomba mtu akufanyia jambo kwa mapenzi/hisani yake. |
| 5.Shukrani | Ni neno linalotumika kuonyesha ishara ya kuridhika kwa jambo la wema ulilotendewa na mtu. |
| 6.Niwie radhi | Ni neno la kuomba msamaha kwa kosa ambalo umemfanyia mtu. |
| 7. Makiwa | Ni tamko la kumfariji aliyepatwa na msiba wa kifo. |

## Maigizo

**Soma maigizo yafuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.**

**Ajok:** Sabakheri poni?
**Poni:** Alkheri! Umeamkaje leo?
**Ajok:** Nimeamka salama salimini poni.
**Poni:** Hata nami nimeamka salama.Waambaje?

**Ajok:** Sina la kuamba.Habari za wengine?

**Poni**: Wote wako salama, nashukuru. Jana jioni nilipofika nyumbani Sikukuona, ulikuwa wapi?

**Ajok:** Ni kweli, nilikuwa nimeenda kumtembelea nyanya kumpa pole. Alikuwa hajihisi vizuri tangu juma lililopita. Je, wajua kuwa nyanya walihama walikokuwa wamejenga awali?

**Poni**: Ndiyo, baba alinieleza kuwa njia ya kwenda kwa nyanya na babu iko upande wa kushoto baada ya kuvuka mto ulio karibu na steni. Aliniambia kuwa nyumba ya nyanya iko karibu na barabara na ina paa ya rangi nyekundu,

**Ajok:** Kweli kabisa.Karibu na nyumba hiyo kuna mti mkubwa ajabu. Tulikubaliana na babu anilaki kwenye mti huo ili nisipotee njia. Nilipofika, nyanya alifurahi sana. Jioni hiyo tulipiga domo mpaka tukaanza kusinzia. Nilimuaga masalkheri naye akaitikia "alkheri".

**Ali:** Ahaa! Nami jana nilikaa na kaka yetu mdogo tukitazama runinga mpaka saa nne. Mara alianza kusinzia na nikampeleka kulala. Nilimuaga alamsiki ijapokuwa alikuwa amelemewa na usingizi.

**Zaina:** Na aliweza kukujibu kweli katika hali hiyo ya usingizi?

**Ali:** Ehe! Alinijibu **binuru** akiwa amefunga macho na mara hiyo hiyo akabebwa na usingizi.

**Zaina:** Hahaha! Watoto na usingizi! Leo mchana, nitamtembelea rafiki yangu Habiba. Ningependa tupange vile tutakavyoanzisha mradi wa vijana.

**Ali:** Unajua kwao?

**Zaina:** La hasha. Alinielekeza kuwa kwao ni magharibi, kilomita kama nane kutoka steni ya magari ambapo atanilaki.

**Ali:** Inaonekana kuwa kwao ni mbali kiasi kutoka steni ya magari. Utaanza safari saa ngapi?

**Zaina:** Ninatarajia kutoka saa sita, adhuhuri. Alinijulisha kwamba atatoka kwao saa nne asubuhi.

**Ali:** Ni kitambo tangu nimwone Habiba. Nitakutuma salamu zangu ukiondoka. Mkumbushe pia kuwa tutakutana mwakani ili tukamwone mjomba aliyepata ajali juzi. Je, utarudi leo ?

**Zaina:** Ndio, nitarudi ifikapo magharibi kabla ya jua kutua. Sipendi

kutembea usiku.

**Ali:** Ni kweli, kuna hatari. Haya siku njema.

**Zaina:** Nawe pia. Nitakujulisha nikiondoka.

## Maswali

1. Taja salamu na mwitikio wake katika mazungumzo yafuatayo:

   **Zaina:** Sabakheri Ali?

   **Ali:** Alkheri Zaina.Umeamkaje leo?

   **Zaina:** Nimeamka salama salimini Ali.

   **Ali:** Hata nami nimeamka salama.Waambaje?

   **Zaina:** Sina la kuamba.
2. Kulingana na kifungu, Ali aliporudi nyumbani jioni Zaina alikuwa wapi?
3. Eleza mwelekeo wa kwenda kwa nyanya kulingana na kifungu.
4. Eleza maana ya nyakati hizi:
   i. asubuhi
   ii. adhuhuri
   iii. magharibi
   iv. alasiri
   v. usiku
   vi. mchana

## Mada Ndogo ya 2: Kusoma

### Shairi

**Soma shairi lifuatalo.**

Amka kumekucha,
Usingizi utupilie mbali,

Mkono mpe mwamkue,
“Jirani **sabalheri?**’’

Jirani jibu kwa furaha,
“**alkheri** jirani yangu,”
Atake kujua na zako,
“Nawe **umeamkaje**?”

Mjibu jirani kwa utulivu,
“**Nimeamka salama salimini,**
**Siku njema** nakutakia,’’
Mtakie wako jirani.

Jibu naye akurudishie,
**‘’Nawe pia** jirani’’
Mazuri tutakiane jameni,
Salamu kiungo cha udungu,
Msalimie mwenzako.

Adhuhuri imefika tena,
Salamu itamalaki hewani,
**Habari za mchana**?
Mwenzangu **umeshindaje**?

Jibu mwenzako umpe,
**Habari za mchana njema**,
**Nimeshinda salama salimini,**
Salamu dawa ya roho.

**Alamsiki** salamu ya usingizi,
**Binuru** majibu mpe mwenzio,
**Usingizi wa pono** mtakie,
**Nawe pia** naye akujibu.

## Maswali

1.Jibu salamu zifuatazoKulingana na shairi

a) Habari za asubuhi?
b) Umeamkaje?
c) Habari za mchana?
d) Umeshindaje?
e) Alamsiki

2.Kulingana na shairi tambua salamu na mwitikio wa:

a) Salamu za Mchana
b) Salamu za usiku

3.Taja salamu nne unazoweza kumwamkua mtu wakati wowote.

# Mada Ndogo ya 3: Sarufi

## Nyakati

**Wakati uliopo -na-**

*Mifano katika sentensi:*

1. Juma a**na**tembea.
2. Mariam a**na**fagia darasa.
3. Mzee Birika a**na**simulia hadithi.
4. Mbunge a**na**tetea jimbo Lake.

**Wakati uliopita -li-**

*Mifano katika sentensi:*

1. Juma a**li**tembea.
2. Mariam a**li**fagia darasa.
3. Mzee Birika a**li**simulia hadithi.
4. Mbunge a**li**tetea jimbo lake.

**Wakati ujao -ta-**

*Mifano katika sentensi:*

1. Juma a**ta**tembea.
2. Mariam a**ta**fagia darasa.
3. Mzee Birika a**ta**simulia hadithi.
4. Mbunge a**ta**tetea jimbo lake.

## Zoezi

**1. Tambua na upigie mstari viambishi vya wakati ujao katika sentensi zifuatazo.**

a) Nini kitamleta kwangu kesho?
b) Jirani hunisalimia kila siku asubuhi.
c) Khadija na Ali wataenda sokoni.
d) Siku hiyo nitalima shamba letu.
e) Walimkimbilia shujaa wao.
f) Watoto wana haki ya elimu.
g) UKIMWI utawaacha watoto wengi mayatima.
h) Atamfikisha karibu na kwao.
i) Ng'ombe alikamwa na mfanyikazi.
j) Kijana alichota maji ya kuoga.

**2. Chagua jibu sahihi kutoka kwenye mabano kujaza mapengo.**

(asubuhi,alheri,usiku,binuru,magharibi,kulia,shikamoo,mchana,kesho,adhuhuri)

a) Siku baada ya leo ni ________.
b) Wakati wa saa sita mchana huitwa ________.
c) Mapema wakati wa kuamka huitwa ________.
d) Unapoambiwa alamski unajibu ________.
e) ________ ni wakati wa jua kutua.
f) Unapofika njia panda unachangua kushoto au ________.
g) ________ ni salamu ya wadogo kwa wakubwa.
h) Wakati baina ya kuchomoza na kutua kwa jua huitwa ________.
i) ________ ni wakati wa kulala.

j) Salamu ya sabalkheri hujibiwaje?

**3. Jaza kifungu kwa neno mwafaka la salamu na wakati.**

Mama alipoamka asubuhi na mapema,alitusalimu ________nasi tukamjibu,“Alheri”.Kakangu alimwamkua,“Shikamoo?”. Naye mama akamjibu ________.Ilikuwa siku yangu ya kupeleka mifugo malishoni mpaka ________yaani saa nane mpaka saa kumi kamili. Nilimuaga mama, “Kwaheri” huku akijibu ________.Baadaye wakati wa ________,jua likitua, nilirudisha mifugo nyumbani.

**4. Geuza maneno yaliyokolezwa wino katika wakati ujao-ta-.**

Mtihani wa somo la Kiswahili **unafanywa** kesho kutwa.Wanafunzi wote **wanatarajiwa** kubeba vifaa vya kuandikia.Kila mwanafunzi **alikuw**a na nakala moja ya maswali.Mwalimu **hutembea** darasani kuhakikisha nidhamu wakati wa mtihani.Wanafunzi **wanafanya** mtihani kwa muda wa saa mbili.Mwalimu **anakusanya** mitihani na **anawapatia** walimu wasahihishe.

**5. Taja wakati wa kuamkuana salamu hizi.**

a) Sabakheri?
b) Binuru!
c) Hujambo?
d) Kwaheri!
e) Safari njema!
f) Makiwa!
g) Pole kwa ugonjwa!
h) Tafadhali!
i) Lala salama!
j) Nisamehe!

**6. Tumia maneno haya kwa usahihi kujaza nafasi.**

(Samahani, pole, asante, Sumile)

a) Ikiwa umemkosea mtu na unataka akusamehe utamwambia _______ au _______.
b) Mwenzako amepata ajali utamwambia _______.
c) _______ni tamko la kurudisha shukrani.
d) _______ nipishe nataka kupita.

## Mada Ndogo ya 4: Kuandika

### Insha

1. Andika kisa juu ya watu wawili wanaotarajia kukutana ili wakawaone watoto yatima.
2. Kwa kutumia msamiati wa salamu andika mazungumzo baina ya:
   a) Mtoto na mzazi
   b) Mjukuu na babu yake
   c) Vijana wawili

# SURA YA 2

## Mada kuu: UHIFADHI WA MAZINGIRA

### Mada Ndogo ya 1: kusikiliza na kuzungumza

**Shairi**

**Soma shairi hili kisha ujibu maswali.**

1. Ufanisi na ukata, asilize mwafahamu,
   Kukosa pia kupata, kipimo chake ni hamu,
   Tafakuri naileta, iwe chanzo cha karamu,
   Tuiache sakata, mazingira tuyatunze,

2. Tukumbuke kuikata, miti ni kujihukumu,
   Maafa tunayaleta, kwa vizazi humuhumu,
   Mvua kutoipata, mazao yawe adimu,
   Tuiache sakata, mazingira tuyatunze,

3. Chemichemi kuzipata, mji uweze kudumu,
   Shiriki pasi kusita, maji yasije gharimu,
   uchafu wote ninateta, nisikilize binadamu,
   Tuiache sakata, mazingira tuyatunze,

4. Moshi kote kunata, maradhi yako timamu,
Magonjwa nayo kutupata, kuishiwa na tabasamu,
wanyama hutawapata, tunawaita haramu,
Tuiache sakata, mazingira tuyatunze.

5. Sikio toeni nta, msije kujidhulumu,
Piganeni hivi vita, vya mazingira adhimu,
usafi nao twaota, maisha yawe matamu,
Tuiache sakata, mazingira tuyatunze,

*(Nukuliwa kutoka kwa WAMBUGU YUSUF,Malenga wa mlimani: Thika.)*

## Zoezi

1.Taja manufaa ya miti kulingana ubeti wa 2.
2.Maneno, "Shiriki pasi kusita, maji yasije gharimu", katika ubeti wa3
yana maanisha nini?
3.Ni madhara gani yanayojitokeza katika ubeti wa 4?

## Mada Ndogo 2: Kusoma

**Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali.**

### UHARIBIFU WA MAZINGIRA

| | |
|---|---|
| **1.**  | **2.**  |
| **3.**  | **4.**  |

Uchafuzi wa mazingira **umekithiri** licha ya wito unaotolewa kila mara na viongozi wetu na wananchi wapenda usafi. Kila mara unapotembea kwenye mitaa ya miji na hata mashambani, unakumbana na **mabiwi** ya taka ambayo yatakufanya uhisi kutapika. Taka za kila aina hukusanyika kwenye maeneo haya na kuwa na vivutio vya jeshi la nzi ambao huja kufaidi uhondo. Bila shaka tunajua hatari za kuwafuga nzi. Wasiojua hatari hizi hujipata wameambukizwa kipindupindu na homa ya matumbo.

Taka zinazotupwa kiholela ni za aina nyingi. Kuna wale ambalo hutupa ovyo vijembe na mikebe ya kila aina. Wengine hutupa sindano zilizotumiwa, misumari na vifaa vingine vya kudungia. Bila shaka taka kama vile mikebe ni makao mazuri ya mbu ambao husababisha malaria. Aidha, watoto wanapocheza karibu na taka hizi huweza kudungwa na misumari yenye kutu na kupata ugonjwa wa pepopunda.

Maendeleo katika sekta ya viwanda yamechangia pakubwa kuongeza uchafuzi wa mazingira. Viwanda vingi **hufusha mioshi** ambayo haichukizi tu bali huweza kusababisha magonjwa ya saratani ya mapafu na pumu. Pia mito mingi imetumika kama majaa ya taka za kila aina kutoka viwanda ni na familia jirani. Licha ya kuwa viwanda husaidia kukuza maendeleo, aina mbalimbali za kemikali kutoka viwandani huishia mitoni. Kemikali hizi hazichafui tu maji bali hutishia maisha za wanyama wa majini kama vile samaki.

Mashambani nako vijito, mito na mabwawa yamegeuka kuwa misala na mabafu ya kuoshea nguo. Si ajabu kuona kuwa unaposafiri kuelekea mashambani itakubidi uyatie macho yako pazia yasione ya kuona. Watu, wazee kwa vijana, huogea kando ya mito na vijito. Maji haya hutumiwa pia kunywa na kupikia.

Mijini mazingira huchafuliwa na magari makuukuuu ambayo, licha ya kutoa moshi mwingi ajabu, hutoa kelele nyingi na kuyaumiza masikio ya wapita njia. Isitoshe, vilabu na maeneo mbalimbali ya starehe hutoa kila aina ya kelele za miziki na za kila sampuli. Ingawa, vijana hufurahia sauti hizi za juu, kelele hizi ni hatari kwani huweza kudhuru **viwambo vya masikio** na kuathiri uwezo wetu wa kusikia.
Aidha, katika sehemu za nyumba za mabanda kuna ukosefu wa misala. Ukosefu huu huwafanya wananchi katika sehemu hizi kwenda haja kokote.

Vyombo vya baharini navyo huvuja mafuta na kudhuru viumbe vya baharini kama vile samaki. Pia kemikali nyingi zinazonyunyuziwa mashamba huweza kudhuru wanaozitumia kemikali hizi na wanyama wanaoishi ndani ya udongo. Kemikali hizi huweza kuua wanyama hawa ambao ndio hurutubisha udongo. Kwa njia hii mazao ya mashamba huathiriwa.

Baadhi ya wananchi kwa sababu ya tamaa ya mali hujenga nyumba ambazo zimesongamana mno. Jambo hili licha ya kutatiza shughuli za uzoaji wa taka, huwatatiza wananchi kwani ni vigumu kupumua hewa safi katika msongamano kama huu.

Pia katika mazingira mengine kama vile shuleni, utakuta kuwa mwanafunzi wengi hutupa karatasi ovyo.Baadhi yao huchonga kalamu zao za mate na kuacha

taka kokote darasani. Wengine hukata nyasi na matawi ya miti na kuyaacha yatapakae kote badala ya kuyachoma. Licha ya uchafuzi wa mazingira, binadamu huyaathiri mazingira yake kwa njia nyingine kama vile kukata miti ovyo na kutopanda mengine. Wengine hulima kandokando ya mito na kuzidisha tatizo la mmomonyoko wa udongo. Baadhi ya wananchi wasiojali hujenga kwenye sehemu zilizotengwa kwa misitu. Wanapokata miti hii kiholela wanasahau kuwa wanazua tatizo la kuenea kwa jangwa.

Kuna wale ambao wameazimia kutafuta riziki zao kwa njia isiyo halali. Hawa nao huwinda na kuwaua wanyama mbalimbali ili wapate nyama na wengine hupata vipusavya vifaru. Ni juu yetu kukumbuka kuwa mazingira ni **tunu** ambayo hatuwezi kuacha ipotee. Tusipoyahifadhi mazingira tutapoteza mengi. Watalii watakoma kuja kututembelea, hawa watalii wasipokuja humu nchini pesa za kigeni zitaendelea kuwa haba na uchumi wetu utadidimia.

*(Nukuliwa toka kwa Kunga za Kiswahili,**na Timothy Arege NA Assumpta Matei**)*

## Zoezi

1. Ni nini kinachotupwa katika mabiwi ya taka kulingana na kifungu?
2. Taja makundi mawili ya watu yanayosisitiza usafi wa mazingira.
3. Taja madhara yanayosababishwa na viwanda.
4. Kulingana na kifungu wanafunzi wanachafuaje mazingira?
5. Wanaowinda wanyama wanatafuta nini?
6. Taja madhara ya kulima kando ya mito.
7. Ni vipi binadamu huchafua mito?
8. Taja magonjwa yanayoletwa na uchafu.
9. Kwa nini watu wanaenda haja popote?
10. Madhara ya kukata miti ni gani?
11. Ukosefu wa watalii utatuathiri kwa njia gani?
12. Orodhesha vitu vinavyochafua mazingira kupitia kwa moshi.
13. Kando na binadamu,ni nani wengine wanaoathiriwa na uchafu wa mazingira?
14. Je, kulingana na kifungu muziki una madhara yoyote?

15. Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu:
    a) umekithiri
    b) mabiwi
    c) huvusha moto
    d) viwambo vya masikio
    e) tunu

## Mada Ndogo 3: Sarufi

### Matumizi ya -nge- na -ngali-

**-nge-** na **-ngali**- hutumiwa kuonyesha utegemeano wa kitu au mtu.Huonyesha hali au jambo linategemea hali au jambo jingine.Kutokea kwa kitendo au hali moja hutegemea jingine.
*Kwa mfano:*
Ningemwona ningemsalimia.
-nge inapotumika mara mbili katika sentensi huonyesha kuwa kitendo cha pili kinategemea kitendo cha kwanza katika kutendeka. Sentensi iliyotumia –nge- huonyesha uwezekano wa kutendeka kwa kitendo.

-ngali- inapotumiwa mara mbili kwa sentensi huonyesha kuwa hapana uwezekano wa kutendeka kwa vitendo vilivyotajwa.

-nge- na –ngali- huonyesha vinavyorejelewa vipo katika wakati uliopita. –nge- na –ngali- hazitumiwi kwa wakati mmoja katika sentensi.

### Kukanusha -nge- na -ngali-

**-nge-** na **-ngali-** hukanushwa kwa kutumia –**si-**.
*Mifano:*
1. Angeenda angemwona.
   A**si**ngeenda a**si**ngemwona. **(Ukanusho)**
2. Angalienda angalimwona.
   A**si**ngalienda a**si**ngalimwona. **(Ukanusho)**

## Zoezi

**A. Eleza maana ya sentensi zifuatazo.**

1. Tungepika tungekula.
2. Msingalikopa tusingalilipa.
3. Mngalikuwa na pesa mngalimpa.
4. Asingeiba asingekamatwa.
5. Ningesoma ningepita mtihani.

**B. Kanusha sentensi hizi.**

1. Angekuja angemwokoa.
2. Wagegombana wangepigana.
3. Tungalisafiri tungalifika.
4. Mngaliimba jana mngalishinda.
5. Angemchukua mtoto huyoangemlea.
6. Ningalisikiliza ningalipona.
7. Angerudi mapema angenisaidia.
8. Wangalishiba wangalilima.
9. Tungemuonya mapema angebadilika.
10. Ningekata tamaa mapema ningeshindwa.

**C. Yakinisha sentensi hizi.**

1. Nisingemkimbilia nisingeanguka.
2. Tusingalikuwa wachoyo tusingali kufa njaa.
3. Mtoto asingalikufa wazazi wasingali huzunika.
4. Kilio kisingalitanda arusi isingalisimamishwa.
5. Mnyama asingepatika,kafara isingefanyika.
6. Tusingalifika mapema tusingalimpata.
7. Msingemtembelea juzi asingelemewa sana.
8. Nisingalilima sana nisingalipata mavuno.
9. Gari lisingemgonga askari wasingekuja.
10. Barua isingeandikwa mapema mwanafunzi asingeenda.

**D. Tumia maneno uliyopewa kutunga sentensi kwa –nge- au –ngali-**

**Kwa mfano:** lima,cheza (-nge-)-Ningelima ningecheza.

1. mwona, lala(-nge-)
2. kimbia,anguka(-ngali-)
3. shona,mpatia(-ngali-)
4. mwonya,nusurika(-nge-)
5. sikiliza,nusurika(-nge-)
6. andika,pata(-ngali-)
7. penda,tuliza(-nge-)
8. choka,choma(-nge-)
9. rukia,okota(-ngali-)
10. rarua,shona(-nge-)

**E.** Tunga sentensi tano kwa kutumia ukanusho wa **-ngali-.**

**F. Tumia msamiati wa mazingiraufuatao kutunga sentensi.**

a) hali ya anga
b) uchafuzi wa mazingira
c) mabiwi
d) kufusha mioshi
e) taka

## Mada Ndogo 4: Kuandika

**Insha**

1. Orodhesha mambo yanayosababisha uharibifu wa mazingira.
2. Andika njia mbalimbali za kuzuia uharibifu wa mazingira.
3. Andika insha juu ya umuhimu wa kuhifadhi mazingira.

# SURA YA 3

## Mada Kuu: UHIFADHI WA WANYAMAPORI

### Mada Ndogo 1: Kusikiliza na kuzungumza

**Shairi**

**Kariri shairi lifuatalo kwa sauti.**

Habari nimesikia,mjini zinatokea,
‘Takuja waheshimiwa,kuja kutembelea,
Na wala sio kukaa,bali kutuona,
Sisi wanyama pori,kweli mwaja kutembelea?

Miji imekua,na mapori yamepanuka,
Wanyama waeza kukaa,huwa wanapendeza,
‘Sema mwaja kujionea hawa,kweli hiyo nia yenu?
Sisi wanyama pori,mwaja kutuua?

Jioni yatimia,mwaendelea kutuona,
Hela nazo mwaleta,nyingi mno mnatoa,
Kwetu mbugani mwaingia,lakini hamtaki kukaa
Sisi wanyama pori,mwaja kututembelea?
Hofu moja tunalo,maisha yetu yamo hatarini,
Japo manufaa mwayapata,kuja kutuona,

Majangili watuwinda,mchana na usiku,
Sisi wanyama pori,mwaja kutuua?

Wengine pembe wataka, wengine kwato zetu,
Misitunitunaogopa, kisha tunajiendea,
Mkija mje na nia, mwaja shida kutatua,
Sisi wanyama pori, mwaja kutuua?
Serekali kilio twatoa,sisi wanyama wote,
Maisha masumbufu yetu,nini tuliwakosea?
Twauliwa kila uchao,hifadhi zetu zatisha,
Sisi wanyama pori, mwaja kutuua?




**Maswali**

1. Kulingana na ubeti wa kwanza wanaokuja wana nia gani?
2. Ni manufaa gani ambayo yanapatikana kwa kuwaona wanyama?
3. Ni nani wanawawinda wanyama pori?
4. Kwa nini wanyamapori wanalalamika katika ubeti wa 5 na 6?
5. Kwa maoni yako mbuga za wanyama pori zina umuhimu wowote?

## Mada Ndogo 2: Kusoma

**Pamoja na mwenzako, tambua wanyamapori hawa.**

| **1.** | **2.** |
|---|---|

| | |
|---|---|
|  **chui** |  **pundamilia** |
| **3.**  **twiga** | **4.**  **Kifaru** |
| **5.**  **duma** | **6.**  **nyati** |
| **7.** | **8.** |

| | |
|---|---|
| <br>**simba** | <br>**fisi** |
| **9.**<br><br>**tembo** | **10.**<br><br>**tumbili** |

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

**WANYAMAPORI**

Wanyamapori ni miongoni mwa rasilimali muhimu na bora kwa maendeleo ya uchumi katika jamii na taifa kwa ujumla.Ni jambo la umuhimu kuwatunza na kuwalinda vizuri dhidi ya majangili ambao huwa wanawaua wanyama hawa kwa lengo la kujipatia kipato wao binafsi pasipo kuzingatia maslahi ya jamii na taifa kwa jumla.Kwa mujibu wa habari, takwimu zinaonyesha kuwa wanyama wanaozidi kupungua sana kila uchao ni tembo na kifaru na hii ni kutokana na hitaji kubwa la malighafi yatokanayo na wanyama hawa kama vile pembe, meno na kwato.

Umuhimu wa wanyamapori katika maendeleo ya uchumi kijamii na taifa ni kuwa huchangia kukua kwa biashara katika jamii.Hii ni kutokana na ongezeko la

watalii kutoka sehemu tofauti tofauti duniani ambayo huja nchini kwa lengo la kujionea wanyama hawa.

Pili, huchangia ongezeko na upatikanaji wa ajira kwa watu, kwa mfano wakalimani, madereva na wapishi.Hii ni kutokana na watu mbalimbali kutembelea hifadhi za wanyama kwani miongoni mwao watalii kutoka nje ya nchi.

Wanyamapori huchangia ongezeko la pato la nchi.Kupitia sekta ya utalii serikali huweza kukusanya mapato kwa mfumo wa kodi zilipwazo na watalii waingiapo nchini na wale wa ndani ya nchi kwa lengo la kujifunza, kuburudika na hata kupumzika.

Mambo muhimu ya kuzingatia ili kuhakikisha wanyamapori wanakuwa salama kwa manufaa ya sasa na kizazi kijacho katika jamii na taifa kwa jumla ni kuhakikisha ulinzi shirikishi baina ya wananchi na serikali kwani watu wanaojihusisha na vitendo vya ujangili wapo katika jamii zetu na tunawajua. Kwa hivyo, hatunabudi kuwavumbua watu hawa kwa manufaa yetu sasa na kwa kizazi kijacho.

Serikali inapaswa kuweka wazi mapato yatokanayo na sekta ya utalii kwa umma. Kwa kutumia njia hii itasaidia watu kuelewa umuhimu wa kuwahifadhi wanyamapori kwani kuna baadhi ya watu hudhani ya kwamba mali au rasilimali hii huwanufaisha watu wachache.

Sheria zilizotungwa dhidi ya majangili ziwe wazi pasipo kupendelea mtu kutokana na wadhifa wake katika jamii na taifa kwa jumla.Endapo sheria zitafuatwa vilivyo wanyama wetu watakuwa salama na hatimaye kupata manufaa makubwa sana katika jamii na taifa.

Hivyo basi, ili tuweze kupiga hatua katika sekta ya utalii hatuna budi kuongeza jitihada za makusudi katika kuhakikisha hifadhi zetu za wanyamapori zinakuwa salama muda wote dhidi ya majangili ambao wamekuwa kikwazo dhidi ya wanyama wetu hali inayosababisha kushuka kwa mapato yatokanayo na sekta hii kila uchao.

## Maswali

1. Kulingana na kifungu wanyama wanaouliwa zaidi ni wepi na kwa nini?
2. Taja manufaa matatu ya wanyamapori kwa taifa lolote.
3. Taja ubinafsi wa wanaowaua wanyama pori.
4. Ni njia zipi ambazo serikali inaweza kuzitumia kukomesha ujangili?
5. Madhara ya kuwauua wanyamapori ni yepi?

# Mada Ndogo 3: Sarufi

## Wakati uliopo na Wakati ujao

### Wakati uliopo

Wakati uliopo **-na-** huonyesha kitendo kinatendeka.Huwa ni wakati huo huo wa kutendeka kwa jambo. Hutumia kiambishi**-na-.**

*Kwa mfano:*

1. A**na**kimbia.
2. Mimi ni**na**imba.

### Wakati ujao

Wakati ujao **-ta-** huonyesha kitendo kitatendeka. Hutumia kiambishi-**ta-.**

*Kwa mfano:*

1. A**ta**kimbia.
2. Mimi ni**ta**enda.

## Zoezi

**A. Jaza jedwali lifuatalo kwa kutumia wakati uliopo na wakati ujao hali ya umoja.**

**Kwa mfano:**kula – Anakula. Atakula.

| Kitenzi | Wakati uliopo | Wakati ujao |
|---|---|---|
| lima | | |
| shuka | | |
| lia | | |
| kimbia | | |
| omba | | |
| fariji | | |
| soma | | |
| ngoja | | |
| osha | | |

**B. Andika sentensi hizi katika wakati uliopo.**

1. Ndugu yangu atatembelea mbuga ya wanyama.
2. Ndovu aliharibu mimea shambani.
3. Nilimwona fisi akila mzoga.
4. Mtoto wa ndege ataitwa kinda.
5. Baba alimpiga picha swara.
6. Nyani wataishi mitini.
7. Wanyamapori watahitaji kulindwa.
8. Msasi ni mtu aliyewaua wanyamapori.
9. Alikamatwa kwa kumuua ndovu yule.
10. Misitu itatumika kama makaazi ya wanyamapori.

**C. Sentensi zifuatazo zimetumia wakati upi?**

1. Watamtembelea lini?
2. Nani anataka kumwona tumbili?
3. Wanamazingira watachunga miti hiyo.
4. Nyoka walipatikana msituni.
5. Mwezi ujao tutapanda miti.
6. Simba anaogopwa na binadamu.
7. Fisi alikula nyama iliyooza.
8. Uhifadhi wa wanyama unafanyika.
9. Ngozi ya chui inatengeneza bidhaa kadhaa.
10. Pembe za ndovu zilipatikana juzi.

**D. Pigia mstari maneno yaliyo na viambishi vya wakati uliopo na ujao katika kifungu hiki.**

Wanyamapori wanapaswa kulindwa kwa kila njia.Wasasi watakaopatikana wakiwawinda wanyama hawa watakamatwa.Nchini mwetu tunahamasishwa juu ya umuhimu wa wanyama hawa wa porini.Binadamu atanufaika kwa kiwango kikubwa kwa kutowaua wanyama hawa.Ninapochunguza faida za kuwahifadhi,ni nyingi mno kuliko hasara.Tunapotembelea mbunga za wanyama,tunafurahia kuwaona.Kizazi kijacho kitanufaika na kuwaona wanyama hawa wa pori.

**E. Andika wakati uliotumika katika kila sentensi.**

1. Mwindaji anaachiliwa lakini atakamatwa.
2. Tumbili anambeba mtotowe na baadaye atapotea.
3. Serikali itajenga ua utakaozuia maangamizi ya wanyama pori.
4. Tumbili watakaovamia shamba lake wanajificha mtini.Mkulima atawawinga ndovu wanaomharibia mazao.

**F. Tunga sentensi saba ukitumia wakati ujao.**

**G. Eleza maana ya msamiati wa wanyamapori ufuatao.**

a) majangili
b) wanyamapori
c) shirika la hudhuma kwa wanyama
d) zuu
e) mbuga za wanyama

## Mada Ndogo 4: Kuandika

## Barua ya kirafiki/kidugu

Barua ya kirafiki huandikwa kwa rafiki au hata kwa mtu wa familia. Unaweza kumwandikia rafiki au ndugu kumjulia hali, kumpongeza, kumpa pole, kumwalika katika sherehe n.k..

**Katika barua ya aina hii, zipo sehemu sita;**

- Sehemu ya kwanza: Anwani ya mwandishi. Anwani huandikwa katika sehemu ya juu ya karatasi upande wa kulia. Katika kuandika anwani, yafuatayo hujumulishwa: Makao ya mwandishi k.m. Shule yake, kijiji chake, mtaa wake n.k; S.L.P. (Sanduku la posta); Nambari ya sanduku la posta apokeapo barua; Mji ambapo posta apokeleapo barua zake ipo; Tarehe aandikapo barua hiyo; Tarehe, mwezi na mwaka.
- Sehemu ya pili: Mkusudiwa. Sehemu hii huonyesha ni nani anayeandikiwa barua k.m. Kwa mpendwa mama/ kaka/ shangazi/mwanangu n.k.
- Sehemu ya tatu: aya ya kwanza au utangulizi wa barua yako. Katika utangulizi yafuatayo huorodheshwa: -Maamkizi -Kujuliana hali -Pongezi labda kwa barua ya hapo awali -Msamaha labda kwa kuchelewa kujibu barua n.k.
- Sehemu ya nne: kiwiliwili Katika sehemu hi, mtahiniwa au mwandishi wa barua, hueleza chanzo cha kuandika barua au sababu.

- Sehemu ya tano: Aya ya mwisho/Tamati. Katika aya hii, mwandishi hutoa salamu kwa watu kadhaa; yaani, hutaka watu hao kufikishiwa salamu zake/humwomba aliyemwandikia kumjibu/huwasilisha jambo lolote. Ni vizuri ujumbe kama huo kuongezewa uzito kwa methali murwa k.m. Ndugu soma kwa bidii kwani elimu ni nguzo aushini; au, jiepushe na anasa kwani mchezea tope huchafuka. n.k.
- Sehemu ya sita. Sehemu hii huwa inaonyesha aliyeiandika barua hiyo. Sehemu hii hufuata tu pindi baada ya aya ya tamati. Huandikwa kulingana na uhusiano wa mwandishi na mwandikiwa wa barua k.m. dada/kaka yako wa toka nitoke, msena wako wa kufa kuzikana, mwanao wa pekee, mama yako mpendwa n.k.

**Mfano wa barua**

Shule ya Wamahiga,

S.L.P 17,

SABASABA.

20-02-2018.

Kwa baba mpendwa,

Zipokee salamu tele kutoka kwangu. Mimi ni mzima na buheri wa afya. Lengo la kukutumia barua hii ni kukujulisha kuwa, wanafunzi wote wa kidato cha pili watafanya ziara katika mbuga ya wanyama pori. Kwa hivyo baba ninakuomba iwapo hali itakuruhusu, unitumie paundi alfu moja. Kiasi hicho kitanitosha kulipia ada ya kiingilio na hata kupiga picha. Mbali na hayo, mimi hapa ninazidi kutia bidii masomoni. Aidha ninazingatia nidhamu. Daima hujaribu juu chini kuzingatia mashauri yako. Kamwe sitaki kusafiria mtumbwi wa mfinyanzi. Tafadhali baba, wasalimie wote nyumbani. Waeleze sina neno na ninawapenda wote. Kwaheri baba mpendwa.

Mwana wako akupendaye,

Poni Ajok.

**Zoezi**

- Mwandikie rafiki yako barua ukimwelezea jinsi ziara kwenye hifadhi ya wanyama pori ilivyokuwa.

# Mada Ndogo ya 5: Msamiati

## Kiimbo

Kiimbo ni sauti maalum inayojitokeza unapotamka maneno fulani na husaidia kuleta maana kamili ya sentensi iliyokusudiwa. Kwa kutamka sentensi kwa sauti fulani 'ya kiwimbo', tunaweza kubainisha kauli ya kawaida, swali, hisia n.k.

Sentensi au maneno yanapotamkwa kwa viimbo mbalimbali, hutoa dhana tofauti. Katika uandishi, Viimbo husaidiwa na alama za uakifishaji ili kumwelekeza msomaji asome kwa kiimbo kilichokusudiwa.

a) Kuulizia Swali (?)

Tunainua sauti tunapouliza swali ili kulitofautisha na sentensi ya kawaida.
k.m Ulisoma kitabu nilichokupatia?

b) Kuonyesha Hisia (!)

Tunapotoa hisia, aghalabu kiimbo huenda juu.
k.m Ajabu!

c) Kutoa Kauli (.)

Tunapotoa kauli (sentensi ya kawaida), aghalabu sauti huenda chini katika neno au silabi ya mwisho. Hata hivyo, sauti inaweza kubadilika kulingana na neno linalotiliwa mkazo katika sentensi.

## Lafudhi

Ni matamshi ya mzungumzaji yanayotokana na lugha yake ya mwanzo, athari za kimazingira au lugha zinazomzunguka.
Udhihirishaji wa sauti za lugha unaomtambulisha mtu mmoja au jamii ya watu.

# SURA YA 4

**Mada kuu: UNUNUZI NA UUZAJI WA BIDHAA**

**Mada Ndogo ya 1:** Kusikiliza na Kuzungumza

**Tambua Vitu hivi vinanyonuluwa dukani na sokoni:**



















**Mazungumzo**

**Soma mazungumzo yafuatayo.**



**Muuzaji:** Hujambo mteja wangu?

**Mteja:** Sijambo sana.Nimezunguka kote katika duka la jumlalako wala sioni bidhaa kadhaa.Naomba unielekeze.

**Muuzaji:** Pole mteja wangu,duka hili ni kubwa sana lakini nitakuonyesha bidhaa zote.Je, ulikuwa unataka bidhaa gani?

**Mteja:** Nilikuwa ninataka sabuni ya maji na ya mti,sukari, chumvi,shati,rinda la mtoto na viatu vyangu.

**Muuzaji:** Oho! Nitakuonyesha bidhaa hizo zote.Kila kitu huwekwa kwenye safu yake.

**Mteja:** Ndio kabisa,nimeona mna mpangilio mzuri wa bidhaa.Unadhifu umedumishwa sana.

**Muuzaji:** Asante sana. Mpangilio wa bidhaa katika safu

unasaidia sana kwa sababu kila bidhaa huwa na bei yake.

**Mteja:** Kweli kabisa.Pia humwezesha mteja kuchagua anachotaka kwa urahisi bila kuchanganyikiwa.

**Muuzaji:** Mteja anapata nafasi ya kuchagua bidhaa kutoka kwa kampuni mbalimbali.Pia unavyoona hatuchanganyi bidhaa kama vile chakula na sabuni.

**Mteja:** Ndio. Ninaona kila sampli ya bidhaa iko katika safu yake.Sababu ni ipi ya kutenganisha bidhaa?

**Muuzaji:** Huwa ni jambo la busara kupanga kwa mfano sabuni mbali na chakula kama mchele,unga hata mboga. Hii inasaidia vyakula visiwe na madhara kama ya sabuni,marashi au hata dawa.

**Mteja:** Kweli kabisa.Sasa nimeona bidhaa zote nilizokuwa nataka.Wacha nichukue kikapu cha kuziweka.

**Muuzaji:** Sawa.Sasa nenda kwa kashia,kaunta ya pili atakuhudumia.

**Mteja:** Asante sana.

**Keshia:** Karibu na uwekelee kikapu hapa nikuhesabie bei.

**Mteja:** Ndio,shika na ukihesabu na mashine yako unanitajia ili nami nihakikishe nimenunua kila kitu.

**Keshia:** Haya.Hapa kuna Sabuni ya maji,sabuni ya mti,nguo ya mtoto shati na sukari.

**Mteja:** Ho!Naona sijachukua viatu vyangu na chumvi.Je, ukiongeza hizo,nikulipe nini?

**Keshia:** Utanilipa pauni 1500.

**Mteja:** Sawa,shika pauni 2000.Je kuna baki?

**Keshia:** Ndio,nitakupa baki ya pauni 500.Shika.

**Mteja:** Asante.

**Keshia:** Karibu tena.


**Maswali**

1. Taja msamiati wa biashara uliotumika katika kifungu.
2. Taja jinsi muuzaji anavyonyesha kujali mteja wake.
3. Kuna tofauti kati ya duka na duka la jumla? Eleza.


4. Je,kuna umuhimu wa kupanga bidhaa katika duka?
5. Kuandika orodha ya bidhaa utakazonunua humsaidiaje mteja?

## Mada Ndogo ya 2: Kusoma


Katika makundi ya wawili wawili, someaneni majina ya wafanyakazi wafuatao na kazi zao.



1.Kinyozi



2. Bawabu




3. Mpishi



4. Mwashi



5. Mwimbaji



6. Seremala




7. Mkulima



8. Mpakaji rangi



9. Mwalimu



10. Muuguzi

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

**ADABU KATIKA MAENEO YA MAUZO**

Ununuzi na uuzaji wa bidhaa ni njia mojawapo ya kukidhia mahitaji.Mtu anapoingia mahali pa kuuzia,iwe ni kibanda,duka,duka la jumla au hata soko anakutana na wateja wengine.Kila mtu huwa anatarajia kununua au kuuza bidhaa.

Wauzaji wengi huwa na mbinu zao za kuwavutia wateja.Utaona matunda yamepangwa vizuri ili kumvutia mteja. Kama ni mboga zitawekwa mahali safi na kulingana na kiwango.Ukitembelea maduka ya mavazi,nguo pamoja na viatu utapendezwa na kila aina ya mitindo. Kuna viatu vya watoto,vijana na hata wazee.Kwa upande wa mavazi,yote ya kiume na kike yanapatikana kwa rangi zote na mitindo anuwai.Kwenye vibanda vya nguo kuukuu utawapata wauzaji na mbinu zao za kuwanasa wateja;muuzaji wa kiume amevaa rinda la mwanamke huku akiimba, “Beba beba! Beba beba! Kumi leo! Kumi leo! Kosa uchekwe!” Kweli kila biashara iko na mitindo yake ya kuuza.

## Tambua biashara hizi

1. 

2. 

3. 

4. 

Mteja anapotaka kununua bidhaa ni lazima kwanza azichunguze. Ikiwa ni mashine ni vyema kukagua ufanyakazi wake.Hii inafanyika kwa idhini na usimamizi wa muuzaji.Usiwahi kwa mfano, kujiwashia mashine kama vile runinga,jiko na nyingine bila ya usimamizi wa muuzaji.Bidhaa kama hizi ziko na utaalamu wake unaojulikana tu na anayeuza.Ukiamua kununua basi ndipo atakapokuonyesha njia za kuziwasha.

Bidhaa nyingine kama vile nguo, viatu, miwani na kadhalika zinahitaji mteja kujipima.Omba idhini kutoka kwa muuzaji kabla ya kujipima kwa kusema, “Tafadhali ninaweza kujipima kiatu,nguo hii?” Hii huonyesha kuwajibika kwa mteja.Ukipewa idhini ni vizuri uchunge sana usije ukaharibu au ukapaka uchafu bidhaa kama hizi.Bidhaa nyingine zinazoweza kuvunjika zinahitaji kukaguliwa kwa uangalifu maana zikivunjika muuzaji ataenda hasara.

Bidhaa hupewa bei kulingana na kiwango na idadi.Mteja anapaswa kuuliza bei ya bidhaa kila mara anapotaka kununua.Pia ni jambo la hekima kuulizia kama kuna aina nyingine za bidhaa unazotaka kununua. Kama vile, “Je, unaweza kuwa na bidhaa nyingine ya aina hii?Kuna bidhaa za rangi nyingine au kiwango kingine?” Hii ni kwa sababu wakati mwingine wauzaji hawana nafasi kubwa ya kuziweka bidhaa zote hadharani.Unapoulizia huenda ukapata nyingine za kupendeza kuliko ulizokuwa umeziona.

Uzaji wa bidhaa unakuwa wa aina mbili;kuna bidhaa ambazo mteja anaweza kujadiliana bei na muuzaji na nyingine bei huwa ni ile tu ambayo imetajwa na muuzaji.Kwa mfano, bidhaa kama sukari,maziwa na kadhalika huwa na bei ya kiwango fulani. Mahali kwingine bidhaa nyingine kama vilenguo,magari, samaki na maharagwe, mteja anaweza kujadiliana bei na muuzaji.Si makosa kumwuliza muuzaji, “Unaweza kunipunguzia bei kidogo mwenzangu?Sina helaunazoitisha. Je, unaweza kuteremshabei ufike kiwango fulani?” Ni jambo la busara kujadiliana bei ili kupunguza gharama.

Mteja anaponunua bidhaa hutoa pesa.Ikiwa pesa zimepita zile za kununua,muuzaji atamrudishia mteja wake baki Lake.Mteja anapaswa kuhesabu baki kuhakikisha liko sawa. Mnunuzi hupata faida yake kutokana na anachouza.Mnunuzi anakuwa makini sana ili asipate hasara kwa kuuza bidhaa zake kwa bei ya chini kuliko inavyotarajiwa.

**Maswali**

1. Taja mahali kutatu kwa kuuzia vitu kulingana na kifungu.
2. Taja mbinu ambazo wauzaji hutumia kuwavutia wateja wao?
3. Toa sababu za kuomba idhini kabla ya kujipima bidhaa fulani.
4. Eleza umuhimu wa kujadiliana beikabla ya kununua.
5. Kwa nini wauzaji hawatoi bidhaa zote hadharani?
6. Sababu ya kurudishiwa baki ni ipi?
7. Faida hupatikanaje?
8. Je, muuzaji anaweza kwenda hasara?
9. Ni tahadhari ipi mteja anapaswa kuzingatia anapokagua bidhaa?
10. Eleza maana ya maneno haya ya ununuzi na uuzaji
    a) bidhaa
    b) bei
    c) pata hasara
    d) baki

**Mada Ndogo ya 3:**

# Sarufi

## Umoja na Wingi wa Nomino

**Nomino** ni jina au majina yanayotumika kurejelea mtu,kitu, hali au mahali fulani.Mfano wa nomino ni duka,kibanda,mkate,muuzaji na kadhalika.Nomino huwa katika umoja na wingi

*Kwa mfano:*

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| mkebe | mikebe |
| kitanda | vitanda |
| mafuta | mafuta |

## Zoezi

**A. Jaza jedwali katika umoja na wingi wa nomino.**

| Nomino kwa umoja | Nomino kwa Wingi |
|---|---|
| ________ | vipimo |
| chumvi | ________ |
| ________ | sukari |
| kinywaji | ________ |
| ________ | mafuta |
| chupa | ________ |
| ________ | pesa |
| tunda | ________ |
| ________ | mboga |
| bidhaa | ________ |
| ________ | wanunuzi |
| duka | ________ |
| ________ | mikate |
| muuzaji | ________ |

| | |
|---|---|
| ________ | sukari |
| unga | ________ |
| | vitanda |
| runinga | _________________________ |
| __________________ | Mikungu ya ndizi |
| mteja | |

**B. Chagua jibu sahihi kwenye mabano.**

1. ________ anauza vitu. (Muuzaji, Mnunuzi)
2. Nyumba kubwa ya kuuzia vitu ni ________.(kibanda,duka)
3. Vitu vinavyouzwa huitwa ________.(bidhaa,mteja)
4. ________ ni kubadilishana pesa kwa vitu. (Kuuza,Kulinda)
5. Mtu ananunua vitu dukani huitwa________.(mteja,kashia).
6. Pesa ambazo hutumiwa kununua vitu huitwa________.(mabaki,bei)
7. ________ ni pesa za juu anazopata muuzaji. (Hasara, Faida)
8. Pesa za juu anazorudishiwa mtu baada ya kununua vitu huitwa ________.(baki,hasara)
9. ________ ni vitu anavyonunua mtu. (Vipimo,Bidhaa)
10. Muuzaji asipozingatia pesa kamili za bidhaa anapata________. (hasara,faida)

**C. Andika katika wingi.**

1. Mkate uliookwa ni mtamu.
2. Mnunuzi alirudisha bidhaa.
3. Maji ya chupa si mazuri.
4. Muuzaji alipata hasara jana.
5. Boga litanunuliwa jioni.
6. Mwanafunzi asiuziwe kinywaji cha kulevya.
7. Mteja aliuliza kipimo cha bidhaa.
8. Kibanda kilibomolewa juzi.
9. Duka kubwa lilihamishwa pale.
10. Baki alilopewa lilipotelea njiani.

## Aina za nomino

Makundi ya kimsingi ya nomino ni sita. Haya ni:

a) Nomino za pekee/maalum
b) Nomino za kawaida
c) Nomino za dhahania
d) Nomino za makundi/jamii
e) Nomino za kitenzi-jina
f) Nomino za wingi

**a) Nomino maalum au nomino za pekee**

Nomino maalum/za pekee:

i. Huanza kwa herufi kubwa.
ii. Hutaja majina ya watu,mahali, mito, milima, maziwa, mabara, mabahari, dini, masomo, siku za wiki na miezi.
*Kwa mfano:*Juma,Halima, Kenya,Sudan Kusini,Mlima Kenya,Bara la Afrika.

**b) Nomino za kawaida**

Nomino za kawaida hutaja vitu vya kawaida.
*Kwa mfano:* kiti,mtu,mnyama,mwana,mwalimu,nyumba, somo na shamba.

**c) Nomino za dhahania**

Nomino za dhahania hutajaa vitu vya kufikiriwa.
*Kwa mfano:* uzuri, harufu, mapenzi, ustadi, mawaidha na urembo.

**d) Nomino za jamii/makundi**

Nomino za jamii/makundihutaja vitu katika makundi.
*Kwa mfano:* tita la kuni,mlolongo wa magari,umati wa watu na bunda la noti.



Shada la maua



Tita la kuni



Bunda la noti



Kichala cha matunda



Mlolongo wa magari



Jozi la viatu

**Soma kifungu kifuatacho kwa makini.**

Kaumu ya watu ilikuwa imengojea kwa hamu na ghamu kumkaribisha rais katika uwanja wa Nyayo. Kigaro cha askari kilipiga foleni huku mlolongo wa magari ya kifahari ya jeshi ukiwa mrefu sana. Punde tu rais alipowasili, kikao cha waimbaji kilimtumbuiza kwa nyimbo mbalimbali. Mara mkururo wa watoto ulijitokeza, watoto wakiwa na shairi la kumkariria rais. Mmoja wao alimkabidhi rais shada la maua .Rais alipendezwa na ushujaa wa watoto hawa. Aliwakabidhi bunda la noti na kusema kuwa zitumike kuwalipia karo ya shule.

**Mifano zaidi:**

1. Kopo la uji au chai
2. Jora la vitenge au vitambaa
3. Robota la pamba
4. Mnofu wa nyama
5. Halmashauri ya shule
6. Doti la leso au kanga
7. Koja la maua
8. Mtungo wa maua

**e) Nomino za kitenzi-jina**

Haya ni maneno yanayoweza kutumiwa kama nomino (majina) au vitenzi. Maneno haya huanza kwa kiambishi Ku-

*Kwamfano:* kucheza, kusoma, kuimba n.k.

**f) Nomino za wingi**

Ni nomino ambazo hutaja vitu ambavyo haviwezi kuhesabika, viko katika hali ya wingi.

*Mifano:* sukari, marashi, mate, wino n.k.

## Zoezi

A) Jaza mapengo kwa kutumia nomino za makundi sahihi.

1. Mnunuzi alituuzia ________ wa samaki, _________ cha zabibu na _________ wa ndizi.
2. ___________ ya shule ilikutana na kutoa mapendekezo ambayo yalipelekewa ______________ la mawaziri.
3. Mhalifu alihukumiwa kifo kwa sababu alikuwa katika __________ la wezi lililoshambulia______________ wa watu.
4. ____________ cha askari kilitawanya______________ ya watu waliokuwa wanaendesha mgomo.
5. Baada ya __________ wa magari kuongozwa katika maegesho, ____________ wa watoto ulifuatia.
6. Mkulima yule amefuga kuku wengi na amefanikiwa na _______________ ya vifaranga.
7. Mkurugenzi alisumbuka sana baada ya kupoteza ___________ cha funguo.
8. Mhazili alinituma posta nichukue ______________ cha barua.
9. _____________ la nguo chafu lilikuwa limerundikwa pamoja kama ____________la nyuki.
10. _________________ ya majaji itakutana kesho kutwa.

## Zoezi

**Pigia mstari nomino katika sentensi zifuatazo.**

1. Dada yangu alienda.
2. Wananchi wote watatembea.
3. Kila mwanafunzi ni lazima asome.
4. Bidhaa zake zimeoza.
5. Nilimuuliza aniuzie vitu vyote.
6. Mashamba yao yalinyakuliwa.
7. Watamtembelea mteja wao.
8. Masomo yakutahiniwa yalipunguzwa.

9. Mchuuzi alizurura sana.
10. Pesa alizokuwa nazo hazitoshi.

**Tambua nomino katika kila sentensi na utaje ni ya aina gani.**

1. Kusoma kuna manufaa mengi.
2. Mto Nile ulifurika mvua iliponyesha.
3. Khamisi alinibebea nilipoumia.
4. Dini yetu inahimiza kusaidiana.
5. Utukutu wake ulimwathiri sana.
6. Mariam anapenda kusoma.
7. Jumamosi ni siku ya kupumzika.
8. Vitabu vya kusoma vimenunuliwa.
9. Muuzaji alinidai nilipomlipa.
10. Maji yakimwagika hayazoleki.

**Nomino iliyopigiwa mstari ni ya aina gani?**

1. Mama alininunulia maziwa**.**
2. Walipoenda kwao walimkuta akila nyama**.**
3. Mlima Kilimanjaroni mkubwa.
4. Uvivu wake utamwangamiza.
5. Maziwa yote yalimwagika.
6. Mtoto alipongezwa kwa bidii masomoni.
7. Seremala Juma alitengeneza viti.
8. Umati wa watuulimzunguka mwalimu mkuu.
9. Barabara ilijaa matopemengi.
10. Nyimbo za Desemba zimetungwa.

## UKUBWA NA UDOGO WA NOMINO

Ukubwa na udogo wa nomino ni kauli ambayo inataja nomino kwa hali iliyo ya wastani.
Nomino zinapobadilishwa kutoka hali ya wastani (kawaida) hadi hali ya ukubwa au udogo, maneno yanayotumika katika sentensi pia hubadilika.

**Mifano;**

Kisu kilimkata mtoto. (Wastani)

Jisu lililikata toto. (Ukubwa)
Kijisu kilikikata kitoto. (Udogo)

Mabadiliko ya nomino kutoka wastani hadi ukubwa huzingatia kanuni kadhaa.

### (a) Nomino zinazoanza na 'm'

Hapa herufi ya mwanzoni huondolewa au hudondoshwa katika baadhi ya maneno.

Mifano;

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. Mtungi | - | tungi | 6. Msafara | - | safara |
| 2. Mpira | - | pira | 7. Mlolongo | - | lolongo |
| 3. Mlango | - | lango | 8. Mchungaji | - | chungaji |
| 4. Mrembo | - | rembo | 9. Msumari | - | sumari |
| 5. Mkeka | - | keka | 10. Mkokoteni | - | kokoteni |

**Mfano katika sentensi:**

1. Mtungi wako umetoboka. (wastani)
   Tungi lako limetoboka. (ukubwa)

2. Mrembo yule alituchezea vizuri.
   Rembo lile lilituchezea vizuri.

3. Mkeka mzuri ulitandazwa kote.
   Keka zuri lilitandazwa kote.

Ukubwa unaodondoshwa herufi 'm' iliyo mwanzoni, pia huzingatia nomino zenye silabi tatu au zaidi.

### (b) Nomino zinazopachikwa 'ji' mwanzoni katika 'ukubwa'

**Mifano;**

| Wastani | Ukubwa |
|---|---|
| 1. Mto | jito |
| 2. Mtu | jitu |

| | |
|---|---|
| 3. Blanketi | jiblanketi |
| 4. Mwizi | jizi |
| 5. Jicho | jijicho |
| 6. Duka | jiduka |
| 7. Kiberiti | jiberiti |
| 8. Shuka | jishuka |
| 9. Gari | Jigari |
| 10. Ziwa | Jiziwa |

**Mifano katika sentensi**

1. Mwizi alipokamatwa alipigwa sana. (Wastani)
   Jizi lilipokamatwa lilipigwa sana. (Ukubwa)

2. Alijifunika shuka kubwa sana. (Wastani)
   Alijifunika jishuka kubwa sana. (Ukubwa)

3. Jiwe hilo linapendeza. (Wastani)
   Jijiwe hilo linapendeza. (Ukubwa)

**c) Nomino zinazoanza kwa kiambishi ‘ki-’ kwa wastani hudondosha ‘ki’ na kupachikwa ‘ji-’**
**Mifano;**

| Wastani | | Ukubwa |
|---|---|---|
| 1. Kiraka | - | Jiraka |
| 2. Kivuli | - | jivuli |
| 3. Kibanda | - | jibanda |
| 4. Kiatu | - | jiati |
| 5. Kisu | - | jisu |
| 6. Kiwiko | - | jiwiko |
| 7. Kikombe | - | jikombe |
| 8. Kidole | - | jidole |
| 9. Kichungi | - | jichungi |
| 10. Kiboko | - | jiboko |

2. Aliokota kiatu kimoja kilichoraruka . (Wastani)
Aliokota jiatu jimoja lililoraruka. (Ukubwa)

3. Tumia kichungi kile kikubwa. (Wastani)
Tumia jichungi lile jikubwa. (Ukubwa)

**(d) Nomino ambazo hudondosha herufi 'm' au 'n' ikiwa nomino zinaanzia ng-, nd-, mb-, nj-.**

**Mifano;**

1. Ngoma - goma
2. Ngumi - gumi
3. Njia - jia
4. Ndizi - dizi
5. Mbuzi - buzi
6. Mboga - boga
7. Ndoo - doo
8. Nguo - guo
9. Mbao - bao
10. Ng'ombe - gombe

**Mifano katika sentensi**

1. Mbuzi wake amejifungua. (Wastani)
Buzi lake limejifungua. (Ukubwa)

2. Nilete maji kwa ndoo hii? (Wastani)
Nilete maji kwa doo hili? (Ukubwa)

3. Ng'ombe wa jirani alipotea. (Wastani)
Gombe la jirani lilipotea. (Ukubwa)

**e) Nomino zinazoanza kwa 'ji' na kupachikwa 'ji' nyingine katika ukubwa**
**Mifano;**

| Wastani | Ukubwa |
|---|---|
| 1. Jino | jijino |
| 2. Jicho | jijicho |
| 3. Jiwe | jijiwe |
| 4. Jina | jijina |
| 5. Jiko | jijiko |
| 6. Jaa | jijaa |
| 7. Jani | jijani |
| 8. Jifya | jijifya |

**(a) Andika kwa ukubwa**

1. Mtungi mweusi umetoboka.
2. Mwuuzaji aliniuzia ndizi mbichi.
3. Rubani aliendesha ndege kubwa.
4. Elimu ya mwanafunzi yule itamfaidi.
5. Ugonjwa wa kipindupindu ni hatari mno.
6. Simba angurumapo, mcheza nani?
7. Mto wa Athi umefurika maji.
8. Milima, misitu na miti ni malighafi ya nchi.
9. Daktari alihimiza watu wale chakula bora.
10. Mwanajeshi alivaa viatu vilivyong'ara sana.

**(b) Andika kwa udogo.**

1. Masichana yalivaa maguo meupe.
2. Mvulana alimgonga nyoka kichwani.
3. Juma alinunua jembe, mwiko na ufagio.
4. Chakula kiliwekwa kwa sahani na kikawekelewa mezani.
5. Matendeguu ya kitanda yamevunjika.
6. Nyumba iliyobomoka haikuwa na madirisha.

7. Mbwa alibeba mfupa wa mbuzi.
8. Mwanamke mvivu alishindwa na kumlaza mtoto.
9. Majijiwe mawili yaliwekwa kwenye njia panda.
10. Mchanga wenye rutuba unafaida nyingi.

### (c) Andika kwa wastani

1. Alijitwika toto gongoni.
2. Kijiti nilichokutana nacho kilinisalimia.
3. Doo lile linavuja.
4. Jitaa la jigari lilivunjika.
5. Jikwe lilinitembelea juzi.
6. Nilinunua kijiko, kijikalamu na kijikaratasi.

### Wakati Uliopo, Wakati Uliopita na Ukanusho

Wakati uliopo hutumia kiambishi **-na-.**
*Kwa mfano:*

1. Tu**na**choka.
2. Tu**na**cheza.
3. Tu**na**soma.

Wakati uliopita hutumia kiambishi–**li-.**
*Kwa mfano:*

1. Tu**li**choka.
2. Tu**li**soma.
3. Tu**li**ona wanyama.

### Kukanusha

Kukanusha ni kukataa. Tunapokanusha, tunatumia kiambishi **HA-**na **SI-.**
*Kwa mfano:*

### Kukanusha wakati uliopo

| | **Yakinifu** | **Kukanusha** |
|---|---|---|
| 1. | Mimi ni**na**choka. | Mimi **si**choki. |
| 2. | Mimi ni**na**cheza. | Mimi **si**chezi. |
| 3. | Sisi tu**na**soma. | Sisi **ha**tusomi. |

## Kukanusha wakati uliopita

| | Yakinifu | Kukanusha |
|---|---|---|
| 1. | Mimi ni**li**choka. | Mimi **siku**choka. |
| 2. | Sisi tu**li**cheza. | Sisi **ha**tu**ku**cheza. |
| 3. | Sisi tu**li**soma. | Sisi **ha**tu**ku**soma. |

## Zoezi

**Chagua sentensi iliyotumia wakati uliopita pekee kati ya sentensi hizi.**

1. Kinara aliitwa na mwalimu.
2. Mchoro anaouchora ni wangu.
3. Rais aliwahutubia wananchi.
4. Basi la shule lilisafirisha wanafunzi.
5. Ugonjwa wa UKIMWI ulimuua mtoto.
6. Imani potovu inapotosha walio na tamaa.
7. Bidhaa ziliuzwa kibandani.
8. Magari yaliyoendeshwa vibaya yatasakwa.
9. Miguu yake huvimba anapovalia viatu.
10. Tulijadiliana bei na mteja aliyetaka kununua shamba.

**Tunga sentensi tano kwa kutumia wakati uliopo.**

**Kanusha sentensi hizi.**

1. Babu yangu alinifunza kuheshimu watu.
2. Kuku wa jirani aliliwa na mbwamwitu.
3. Nilihudhuria arusi yake huko kijijini.
4. Nguo za mtumba zina bei nafuu.
5. Meli ya tatu inabeba mizigo yote.

## Mada Ndogo ya 4: Kuandika

**Barua rasmi**

Katika biashara mtu anaweza kuandika barua kwa muuzaji juu ya mambo yanayohusiana na shughuli za biashara.Inaweza kuwa ni kuagiza bidhaa fulani, kushukuru au kulalamika.Barua hiyo huwa ni rasmi. Kwa hivyo, huchukua muundo wa barua rasmi. Barua rasmi huwa na:

1. Anwani ya anayeandika.
2. Anwani ya anayeandikiwa.
3. Mintarafu au sababu ya kuandika.
4. Mwili/ujumbe wa barua.
5. Kimalizio chenye sahihi
6. Jina la mwandishi.

**Soma barua ifuatayo.**

Mwanaisha Abubakar,
Sanduku La Posta 02,
KITENGO
12/7/2017.

Kwa Mkurugenzi,
Kampuni ya LITZO
SLP 96,
KITENGO.

Kwa Mkurugenzi,

**MINT: KULALAMIKIA BIDHAA GHUSHI**

Nakuandikia barua hii kulalamika juu ya mashine zilizowasilishwa katika duka langu juma lililopita.Katoni mbili kati ya kumi zilikuwa na mashine ghushi.Mashine hizi ni za zamani sana na zimepitwa na wakati. Mashine hizi pia hazina mhuri wa Kampuni yako. Siwezi kuthibitisha kama ni za kampuni yako. Ninaomba uzijie mashine hizi leo na uniletee nyingine kulingana na makubaliano yetu.

Wako mwaminifu,
Mwabukar

MWANAISHA ABUBAKAR.

## Zoezi

1. a) Ni nani ameandika barua hii?
   b) Nani aliyeandikiwa barua hii?
   c) Ametoa sababu gani za kuandika barua hii?
2. Taja malalamishi mawili ya mnunuzi kulingana na barua.
3. Andikia kampuni fulani barua ukiagiza bidhaa.

## Mada Ndogo ya 5: Msamiati

### Tarakimu

**Tarakimu ni alama ya hesabu iliyoandikwa kuonyesha idadi.**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1 moja | 2 mbili | 3 tatu | 4 nne | 5 tano |
| 6 sita | 7 saba | 8 nane | 9 tisa | 10 kumi |
| 11 kumi na moja | 12 kumi na mbili | 13 kumi na tatu | 14 kumi na nne | 15 kumi na tano |
| 16 kumi na sita | 17 kumi na saba | 18 kumi na nane | 19 kumi na tisa | 20 ishirini |
| 21 ishirini na moja | 22 ishirini na mbili | 23 ishirini na tatu | 24 ishirini na nne | 25 ishirini na tano |
| 26 ishirini na sita | 27 ishirini na saba | 27 ishirini na nane | 29 ishirini na tisa | 30 thelathini |
| 31 thelathini na moja | 32 thelathini na mbili | 33 thelathini na tatu | 34 thelathini na nne | 35 thelathini na moja |
| 36 thelathini na moja | 37 thelathini na saba | 38 thelathini na nane | 39 thelathini na tisa | 40 arobaini |
| 41 arobaini na moja | 42 arobaini na mbili | 43 arobaini na tatu | 44 arobaini na nne | 45 arobaini na moja |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 46 arobaini na moja | 47 arobaini na saba | 48 arobaini na nane | 49 arobaini na tisa | 50 hamsini |
| 51 hamsini na moja | 52 hamsini na mbili | 53 hamsini na tatu | 54 hamsini na nne | 55 hamsini na tano |
| 56 hamsini na sita | 57 hamsini na saba | 58 hamsini na nane | 59 hamsini na tisa | 60 sitini |
| 61 sitini na moja | 62 sitini na mbili | 63 sitini na tatu | 64 sitini na nne | 65 sitini na tano |
| 66 sitini na sita | 67 sitini na saba | 68 sitini na nane | 69 sitini na tisa | 70 sabini |
| 71 sabini na moja | 72 sabini na mbili | 73 sabini na tatu | 74 sabini na nne | 75 sabini na tano |
| 76 sabini na sita | 77 sabini na saba | 78 sabini na nane | 79 sabini na tisa | 80 themanini |
| 81 themanini na moja | 82 themanini na mbili | 83 themanini na tatu | 84 themanini na nne | 85 themanini na tano |
| 86 themanini na sita | 87 themanini na saba | 88 themanini na nane | 89 themanini na tisa | 90 Tisini |
| 91 tisini na moja | 92 tisini na mbili | 93 tisini na tatu | 94 tisini na nne | 95 tisini na tano |
| 96 tisini na sita | 97 tisini na saba | 98 tisini na nane | 99 tisini na tisa | 100 mia moja |

## Zoezi

### Andika kwa maneno.

1. 34 ________________________
2. 21 ________________________
3. 3 ________________________
4. 18 ________________________
5. 25 ________________________
6. 17 ________________________
7. 6 ________________________
8. 93 ________________________
9. 88 ________________________
10. 11 ________________________

**Mkiwa kwa makundi ya wawili wawili, someaneni michoro ifuatayo.**




Bank of
South Sudan
Promise to pay the bearer on demand
AB8075922
Five
South Sudanese
Pounds
Governor
Minister of Finance
5


Bank of
South Sudan
Promise to pay the bearer on demand
AJ5815033
Ten
South Sudanese
Pounds
Governor
Minister of Finance
10


Bank of
South Sudan
Promise to pay the bearer on demand
AA8289172
Twenty
South Sudanese
Pounds
Governor
Minister of Finance
2015
20


50
Bank of
South Sudan
Promise to pay the bearer on demand
AB2431609
Fifty
South Sudanese
Pounds
Governor
Minister of Finance
Dr. John Garang de Mabior


100
Bank of
South Sudan
Promise to pay the bearer on demand
AA9156813
One Hundred
South Sudanese
Pounds
Governor
Minister of Finance
2015

# SURA YA 5

## Mada kuu: AFYA NA MAGONJWA

### Mada Ndogo ya 1: kusikiliza na kuzungumza

**Shairi**

**Soma shairi hili.**

Hodi hodi twaingia, twaja na letu shairi,
Shairi kuwaletea, sikiliza kwa makini,
Leo tutawaambia, mti ukunje uli maji,
Tukapime afya zetu, afya zetu ziwe bora.

Nchi yaingia shida, saratani inabisha hodi
Magonjwa ‘siyo na tiba, shinikizo la damu linazidi
Washauri wanasaha, ushauri wautoa
Tukapime afya zetu, afya zetu ziwe bora

UKIMWI gonjwa hatari, UKIMWI waua wengi
Kupimwa ni tahadhari, tuishi kwa tumaini
Kina mama kina baba, vishawishi epukeni,
Tukapime afya zetu, afya zetu ziwe bora.

Wapendwa viongozi wetu,watangaza kote kote
Watu wote wakapimwe,afya zetu tufahamu
Jambo moja ni muhimu,ushauri kuupata
Tukapime afya zetu, afya zetu ziwe bora.

Wewe utaishi vyema,na kazi utazifanya
Kupima usiogope,ndiyo mwanzo tumaini
Viongozi mkapimwe,Mungu awajalieni
Tukapime afya zetu, afya zetu ziwe bora.

Watoto msituache, twapenda nayo masomo
Tukijua ni hakika,elimu bora kupewa,
Na tukapimwe afya zetu, afya zetu ziwe bora.
Tukapime afya zetu, afya zetu ziwe bora

Ua baya haliliki, hata nyuki hutapika
Nasi tungekuwa nyuki, madhara kuyaepuka
Nchi zingejaa haki, madhara kuyaepuka
Tukapime afya zetu, afya zetu ziwe bora

## Zoezi

1. Taja ujumbe unaojitokeza katika shairi hili.
2. Mshairi anaposema "mti ukunje ungali mbichi" anamaanisha nini?
3. Kwa nini mshairi anahimiza watu wakapimwe?
4. Taja mifano minne ya wale wanaopaswa kupimwa.
5. Eleza maana ya ndani ya:
    a) Ua baya haliliki, hata nyuki hutapika
    b) Nasi tungekuwa nyuki, madhara kuyaepuka

**Mada Ndogo ya 2:** **kusoma**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**



**MISINGI YA KUWA NA AFYA NJEMA**

Afya njema ndio msingi wa kila kitu. Kuwa huru dhidi ya magonjwa kunasaidia kukupa nguvu na nafasi ya kuweza kufikiria zaidi na kufanya vizuri zaidi kazi zako.

Hakuna mtu anayependa kuumwa, ila inatokea tu tunajikuta tuna magonjwa na matatizo mengine ya kiafya; aidha kwa kutarajia au pasipo kutarajia. Kuna mambo kadha wa kadha ambayo mtu anaweza kuyafanya ili kuweza kuuweka mwili wake vizuri na kuwa na afya njemaama kwa kutoumwa na magonjwa au kwa kuweza kudhibiti ugonjwa wake vizuri.

Jambola kwanza, unaweza kuwa na afya njema kwa kula chakula bora na cha kutosha. Ni vizuri kuuzoesha mwili wako matunda, asali, maziwa, viungo-dawa kila siku.Vyakula hivi vinajenga mwili na kuukinga dhidi ya uvamizi wa virusi vyovyote vile.Usizoee kula aina moja ya vyakula.

Jambo la pili ni kufanya mazoezi ya kutosha. Unapofanya mazoezi mwili unatokwa na jasho.Jambo hili husaidia vishimo vidogo vilivyoko kwenye ngozi kufunguka na kupata hewa safi. Mazoezi husaidia usafirishaji wa damu kwenye mishipa.Mazoezi ya mwili huchoma mafuta yaliyokwamia mishipani.

Afya nzuri hupatikana kwa kupumzika vya kutosha.Mwili ni kama mashine yoyote;ukiifanyisha mashine kazi bila kuipumzisha,itajipumzisha kwa kukataa kazi!Mwili nao uko hivyo,usipoupumzisha utakuwa mgonjwa na kukataakufanya chochote.Ni vizuri kupumzisha mwili kwa kulala usingizi wa kutosha; angalaumuda wa saa saba kila siku.Hii itakupa nguvu ya kuendelea na shughuli zako ukiwa na afya.

Kunywa maji safi.Maji husaidia wepesi wa kusaga na kusafirisha chakula mwilini.Ukikosa kunywa maji ya kutosha unaunyima mwili wako kitu muhimu sana.

Utumiaji wa chumvi, sukari na mafuta kwa kiasi kikubwa huathiri afya.Punguza ulaji wa chumvi, sukari na mafuta.Tumia kiasi kidogo cha chumvi, sukari na mafuta. Epuka vyakula na vinywaji vyenye chumvi na sukari nyingi.

Afya nzuri ni mwili usio na maumivu.Jikinge dhidi ya magonjwa, ajali na vitu vingine vinavyoharibu afya yako.Jua jinsi ya kujikinga dhidi ya magonjwa, ajali na vitu vingine vinavyoharibu afya yako kama sumu,vipodozi, vyakula na vinywaji visivyo salama.Wakati mwingi mtu anajikuta anakunywa vinywaji vilivyotengenezwa na hajui asili yavyo;vingine huwa vimechanganywa na rangi tu kuzipa ladha na rangi.

Dhibiti uzito wa mwili wako. Uzito wa mwili hutegemea kiasi cha sukari na mafuta mwilini.Uzito uliopita kiasi kinachotakikana na mwili wako utakuweka katika hatari ya kupata magonjwa ya kisukari, presha, moyo na kadhalika.

Dhibiti uzito wako vizuri.Msongo au fikira nyingi pia huweza kukusababishia magonjwa ya moyo, presha na kadhalika. Kabiliana vizuri na msongo wa mawazo.

Mwisho, elimu na ushauri wa kinsi ya kuweza kujikinga dhidi ya magonjwa au kuishi vizuri na ugonjwa ni muhimu sana.Ukiumwa, pata matibabu kabla hali haijawa mbaya zaidi.Soma,sikiliza na hudhuria mikutano inayofunza juu ya afya na utanufaika.


## Maswali

1. Chakula kinasaidiaje kuwa na afya njema?
2. Taja umuhimu wa maji.
3. Ni magonjwa yepi yanayoletwa na uzito mwingi wa mwili?
4. Taja njia **tano** za kuwa na afya njema kulingana na kifungu.

## Shughuli ya ziada

## MALARIA NA KIFUAKIKUU

**Soma taarifa ifuatayo.**



Malaria na kifuakikuu, yaani *TB*, ni magonjwa ambayoyametambulika kuwauwa watu wengi sana.Magonjwa haya yanatishia mamia ya watu katika maeneo mbalimbali ulimwenguni.Watu wengi wanakabiliwa na hatari ya kuambukizwa.Malaria ni ugonjwa unaosababishwa na vimelea.Vimeleavinavyosababisha malaria huingia katika mfumo wa damu kupitia kuumwa na mbu jike.

Vimelea hivyo huenda katika chembe za ini la mtu aliyeambukizwa.Vimelea huzaana.Wakati chembe nyekundu za damu zinapopasuka, huruhusu vimelea ambayo hushambulia kwa wingi zaidi chembe nyekundu za damu ya mtu.Vimelea hivi huzidi kuongezeka.Dalili zake ni pamoja na homa, kuhisi baridi, kutokwa na jasho, maumivu ya kichwa na mwili, kichefuchefu, na kutapika, kuhisi joto kali, kutetemeka kwa mwili, maumivu ya misuli na kuendesha.

Njia za kujikinga kuambukizwa malaria ni pamoja na kutumia neti iliyowekwa dawa ya kuua mbu na isiwe na shimo au tundu. Hakikisha umechomeka neti yenyewe vizuri kwenye godoro ili mbu asipate mwanya wa kukuvamia wakati umelala.Pili, puliza dawa ya kuua wadudu nyumbani mwako na ikiwezekana weka wavu wa kuzuia wadudu katika madirisha na milango na utumie kiyoyozi na feni kuwafukuza mbu.Vaa nguo zenye rangi angavu na zinazofunika mwili vizuri.Inapowezekana, epuka kuwa katika maeneo yenye mbu wengi, mabwawa yenye mbu, na maji yaliyotuama; mahali ambapo mbu huzaliana.

Ikiwa unapanga kutembelea nchi ambayo malaria imeenea, kabla ya kusafiri, pata habari za karibuni kuhusu ugonjwa huo kwani aina ya vimelea vya malaria wa eneo moja huenda vikatofautiana na vya eneo jingine. Jambo hilo litakusaidia kuamua aina ya dawa inayofaa zaidi. Aidha, litakuwa jambo la hekima kuwasiliana na daktari wako ili kujua mambo unayopaswa kuepuka kwa kuzingatia hali ya afya yako.

Tumia dawa zilizothibitishwa na mamlaka kwani kutumia dawa zisizofaa au dawa bandia kunaweza kuzidisha ugonjwa na kuhatarisha uhai.Ondoa vitu vyovyote vinavyozunguka nyumba kama vile mikebe, chupa na mitungi wazi vinavyoweza kuwafanya mbu kuzaliana.Ikiwa unaishi katika eneo lenye

ugonjwa wa malaria au umewahi kutembelea eneo lenye ugonjwa huo, usipuuze daliliza malaria.Ugonjwa wa malaria usipotibiwa unaweza kusababisha upungufu wa chembe za damu na hivyo kuhatarisha uhai. Kabla ya dalili hizo kuwa mbaya hata zaidi, tafuta matibabu haraka, hasa inapohusu watoto na akina mama wajawazito.

Kifua kikuu au *TB* ni ugonjwa unaosababishwa na vimelea ambayo inaweza kuingia kwa binadamu na kusababisha madhara katika sehemu yoyote ya binadamu. Vimelea hii, kwa mfano, inaweza kuathiri mtu kwenye mapafu, figo, katika utumbo, ngozi, ubongo na kwingineko.

Njia kuu ya kuenea kwa vimelea hii ni kwa kuvuta hewa yenye wadudu hao. Hii ni kutokana na kuishi au kuwa karibu na mtu mwenye ugonjwa huo. Mtu huyo anapopiga chafya au kukohoa bila kufunika mdomo ndipo unapoweza kuambukizwa wadudu hao.Vimelea hii pia husababishwa kwa kula vyakula visivyopikwa vikaiva vizuri. Watu wanaokunywa maziwa ambayo hayajachemshwa pia wako katika hatari ya kupatwa vimelea hao.

Ugonjwa huu unaweza kumshika yeyote.Kundi ambalo liko kwenye hatari kubwa ya kuambukizwa kifua kikuu ni la wale wanaoishi kwa karibu na kwa muda mrefu na mtu yule aliyekwisha kuambukizwa ugonjwa huo na ambaye bado hajaanza matibabu. Wengine niwatoto wadogo na wazee; wale wote wanaougua kisukari; watu wanaotumia dawa zinazoathiri mfumo wa kinga ya mwili; waathiriwa wa UKIMWI, wale wote wanaoishi maeneo yenye msongamano mkubwa wa watu; wanaoishi kwenye sehemu zisizokuwa na hewa ya kutosha; watu wanaotumia dawa mbalimbali au pombe na mwisho wale wenye lishe duni.

Dalili za ugonjwa wa kifua kikuu huwa ni pamoja na Kikohozi cha muda mrefu kama wiki mbili au zaidi,kukohoa damu,homa isiyoisha;hasa homa ambayo inapanda sana wakati wa usiku ikiambatana na kutokwa jasho jingi wakati wa usiku kiasi cha kulowesha mashuka;kupungua uzini kusiko kwa kawaida na pia maumivu ya kifua wakati wa kukohoa. Dalili nyingine ni kukosa hamu ya kula, kuchoka na kutokwa jasho wakati wa usiku.Mtu anaweza kuzuia kifua kikuu kwa njia zifuatazo.

Kama tayari ameambukizwa *TB*, ahakikishe anapokohoa au kupiga chafya anafunika mdomo wake ili kuepuka kumuambukiza mwingine. Anapotema mate ahakikisheanayafukia vizuri.Aende hospitalini kupata matibabu mapema.Nenda hospitali mara unapokuwa na dalili zinazofanana zilizotajwa ili kujihakikishia afya yako na kuanza tiba mapema ilmuradi usiwaambukize watu wengine.

## Maswali

1. Kifungu hiki kimeshughulikia magonjwa yepi?
2. Taja njia za kuambukizwa;
   a) Ugonjwa wa malaria
   b) Ugonjwa wa kifuu kikuu.
3. Taja dalili sita za:
   a) ugonjwa wa malaria
   b) ugonjwa wa kifuakikuu
4. Unawezaje kujizuia na Malaria?Taja njia nne.
5. Je, kuna madhara ya kujitibu kwa kununua dawa za Malaria?
6. Usafi wa mazingira ya boma husiadia kuondoa mbu.Taja usafi huu.
7. Ushauri wa kutopatwa na malaria unapoenda maeneo tofauti na yako ni upi?
8. Vimelea ya kifuakikuu inaathiri sehemu zipi?
9. Taja njia ambazo mtu mwenye kifuakikuu anaweza kuambukiza wengine.
10. Chakula kinaweza kusababisha kifua kikuu? Eleza.
11. Orodhesha makundi yaliyo katika hatari ya kuambukizwa kifuakikuu.
12. Taja njia zote zilizotajwa za kuzuia kuambukiza kifua kikuu.
13. Kwa nini ni muhimu mtu anapoona dalili za TB aende hospitali?
14. Taja dalili ambazo ni sawa kwa mtu mwenye malaria na yule mwenye kifuakikuu.
15. Tunga sentensi ukitumia maneno haya:
    a) kuambukizwa
    b) chandarua
    c) kupuliza dawa
    d) kupiga chafya
    e) dawa bandia

**KIFUNGU B**

## UKIMWI

**Simulia wenzako kisa hiki kwa sauti.**

Katika kijiji kimoja kulikuwepo na mama mmoja aliyekuwa na mifugo wake; kuku, mbuzi na ng’ombe. Katika nyumba yake kulikuwa na panya.

Mama huyu alikuwa akisumbuliwa sana na panya. Kwa hivyo, aliamua kununua mtego kwa lengo la kuwamaliza hao panya. Panya wakawa wananaswa na ule mtego na kufa kila siku. Panya hawakuwa na uwezo wa kuondoa ule mtego.

Panya walifikiri kwa kina na kuona wanapungua siku hadi siku. Panya mmoja alimwendea kuku kumwomba wasaidiane kuondoa mtego huo maana wenzake wanamalizika. Kuku alimwuliza, “Je, umewahi kuona hata kuku mmoja amenaswa na huo mtego?’’

Panya alijibu kuwa hapana. Kuku alimwambia kuwa basi mtego huo haumhusu yeye.

Panya alivumilia lakini aliona haiwezekani. Heri aende kwa mbuzi. Panya alimwambia mbuzi, “Haloo mbuzi! Wewe ni hodari na una nguvu sana.Unaonaje ukinisaidia tukauondoe huo mtego, maana wenzenu tunamalizika?’’
Mbuzi alijibu, “Umewahi kuona hata mbuzi mmoja amenaswa katika mtego huo?”
Panya alijibu kuwa hapana.
Mbuzi alimwambia, “Basi huo mtego haunihusu mimi.”
Panya bado aliendelea kusugua kichwa. Alimwendea ng’ombe na kumwomba. Majibu yalikuwa yale yale.

Siku moja usiku, yule mama alisikia kelele kama za panya aliyenaswa katika ule mtego. Alizungusha mkono wake ili kutafuta kibatari na kibiriti ili awashe na kumuua panya aliyenaswa kwenye mtego. Mara alisikia kitu kimemng’ata mkononi. Alipowasha kibatari kumbe alikuwa nyoka mkubwa ambayealinaswa mkia wake kwenye mtego wa panya.

Sumu ya nyoka iliendelea kuenea katika mwili wa mama huyo. Baadaye, mama huyo alipelekwa hospitalini. Hata hivyo, hali yake ilizidi kuwa mbaya, wakasema jamani mchinjeni kuku, mama apate supu. Kwa hivyo, kuku alichinjwa.Hali ya mgonjwa ikaendelea kuwa mbaya zaidi wakasema mchinjeni mbuzi, nyama iuzwe tupate fedha kwa ajili ya matibabu. Mbuzi alichinjwa.

Hali ya mgonjwa ikawa mbaya zaidi hadi akapoteza maisha. Watu wakaja wengi kwenye msiba. Mboga zilihitajika. Walisema watu ni wengi sana kwa hivyo ng'ombe achinjwe. Ng'ombe naye alichinjwa. Kwa hivyo, wote ambao mtego haukuwahusu uliwasababishia vifo ingawa wao waliona ni panya tu mhusika.

Hivyo basi, mtego wa panya ni sawa na ugonjwa wa UKIMWI ambao tunauona upo mbali na sisi aukwa jirani lakini tusipokuwa makini, unaweza kuwapo hata kwetu pia. Tusiwabague waathiriwa wa ugonjwa wa UKIMWI.

## Zoezi

1. Mama alinunua mtego kwa nia gani?
2. Kwa nini panya walishindwa kuuondoa mtego wa mama?
3. Taja wahusika waliokataa kumsaidia panya.
4. Kwa nini ng'ombe alichinjwa?
5. Kisa hiki kinatufunza nini?

## KIFUNGU C

### KANSA





Kansa au kwa jina jingine saratani, ni kundi la magonjwa yanayosababishwa na mgawanyiko usio sawa na usiodhibitika wa seli na kuunda uvimbe unaovamia na kuzidhuru tishu mwilini.Kansa huanza wakati seli katika sehemu mojawapo ya mwili zinapoanza kukua bila kudhibitiwa. Ukuaji wa seli za kansa hutofautiana na ukuaji wa kawaida wa seli za mwili na badala ya kufa pale zinapozeeka huendelea kukua na kuzaa seli nyingine mpya zisizokuwa za kawaida.Kwa hiyo, kukua kusikodhibitiwa na kusiko kwa kawaida kwa seli, na tabia ya seli hizo kuzishambulia tishu nyingine ndiko hasa husababisha seli za kansa.

Si kila uvimbe ni kansa bali kuna uvimbe ambao si kansa. Uvimbe huu huweza kugawanyika na kukua. Hutengeneza mirija mipya ya damu ili kujipatia lishe wenyewe. Hata hivyo, uvimbe huu usiokuwa kansa, unaweza kuleta matatizo kama vile kukua sana na kuvibana viungo na tishu nyingine mwilini. Aidha, uvimbe kama huu huweza kukua na kubadili utendajikazi wa mwili.

Hata hivyo, aina zote za kansa zina sifa tatu zinazofanana. Sifa hizo ni ukuaji wa seli usiodhibitika, uwezo wa kuvamia na kushambulia tishu nyingine na uwezo wa kusambaa katika viungo vingine mwilini kupitia mishipa ya damu. Baadhi ya kansa huwashambulia zaidi wanawake, kwa mfano kansa ya matiti na kuna baadhi ambazo huwashambulia zaidi wanaume.Baadhi ya kansa huwashambulia watu wa kundi fulani katika jamii kutokana na aina yao ya maisha au kazi wanazofanya kila siku. Hali kadhalika kuna baadhi ya kansa au saratani zinazowashambulia watoto zaidi kuliko watu wazima kwa mfano kansa ya damu.

Kuna aina za kansa kama vile saratani ambayo hushambulia viungo mbalimbali vya mwili vilivyo ndani na njekama vile mapafu, matiti, utumbo na kadhalika. Kuna saratani inayopatikana kwenye mifupa, misuli na tishu mbalimbali mwilini. Saratani nyingine huanza kwenye tishu za kinga ya mwili.Kuna saratani zinazoanza ndani ya ute wa mifupa na kukusanyika kwenye mishipa ya damu.

Asilimia kubwa ya magonjwa yote ya kansa yanahusishwa zaidi na mtindo wa maisha ambao vipengele vyake ni ulaji, kutofanya mazoezi ya mwili na matumizi ya pombe na tumbaku. Vitu vingine vinavyochangia ni pamoja na virusi na vimelea, madini mazito, mionzi na sumu.

Vyakula huchangia kwa kiasi kikubwa saratani za kinywa na koo, matiti, tezi za kiume, utumbo mpana, mapafu, tumbo, ini, kongosho na kizazi. Ulaji unaoweza kuchangia ugonjwa huu ni wa nyama nyekundu kupita kiasi, nyama zilizosindikwa, vyakula vilivyokuzwa kwa kemikali nyingi kama mbolea, vyakula vyenye mafuta mengi ambavyo huweza kusababisha uzito mwingi na vyakula vilivyoota ukungu, kwa mfano, karanga.Ulaji wa nyama nyekundu, kwa mfano ya ng'ombe unaongeza uwezekano wa kupata saratani ya utumbo mkubwa.Nyama zilizosindikwa pamoja na zile zilizohifadhiwa kwa kuongezwa chumvi, mafuta, kemikali au kukaushwa kwa moshi kama nyama za kopo, soseji na bekoni zinaongeza sana uwezekano wa kupata saratani. Hakuna kiasi chochote cha nyama iliyosindikwa kinachoweza kutumika bila kuongeza uwezekano wa kupata saratani.

Viazi vya kukaanga mfano viazi mviringo huongeza hatari ya kupata saratani hasa vikikaangwa kwenye mafuta. Vinywaji baridi au laini kama vile soda na juisi za viwandani navyo vinaweza kusababisha kansa. Utafiti uliofanywa unaonyesha kuwa mtu aliyetumia soda mbili au zaidi ndani ya wiki moja ana uwezekano wa kupata saratani.

Tafiti nyingine zimeonyesha uhusiano kati ya matumizi ya sukari na saratani za tumbo na utumbo mpana ingawa sukari haifanyi seli nzuri zisizo na kasoro kuwa kansa ila sukari ni chakula ama chanzo cha lishe ya seli za kansa. Pombe inaongeza sana uwezekano wa kupata saratani hasa zile za koo, kinywa, ini, mapafu na matiti.

Uzito uliozidi kiasi unamweka pia mtu kwenye hatari ya kupata magonjwa mengi sugu, kama vile kisukari, msukumo wa damu, magonjwa ya moyo, figo na saratani za matiti, kongosho na kizazi. Utaratibu mzuri wa kula, husaidia kupunguza uzito au kuzuia ongezeko kubwa la mwili.

Wataalamu wanashauri kwamba hatari ya kupatwa na kansa inaweza kupungua kwa kubadilisha mtindo wa maisha ya mtu binafsi, kama vile kujiepusha na uvutaji wa sigara, kujiepusha kukaa juani kwa muda mrefu, kula lishe bora na kufanya mazoezi mara kwa mara.

Aidha, vyakula vitokanavyo na mimea ni kinga nzuri ya kuzuia saratani. Kutumia zaidi vyakula vitokanavyo na mimea husaidia kuondoa uwezekano wa kupata saratani za aina mbalimbali. Inashauriwa kula angalau vipimo vitano vya mboga mbalimbali kwa siku.

Hakikisha katika kila mlo unaotumia kunakuwa na nafaka zisizokobolewa kama vile unga wa ngano usiokobolewa sana, unga wa dona, mchele wa brauni, ulezi na aina mbalimbali za mikunde kama vile maharage, kunde, choroko na mbaazi. Mazoezi ya mwili yanapaswa kuwa sehemu ya maisha ya kila siku.

Kansa inaweza kudhibitiwa kwa kudhibiti usambaaji wa seli za kansa   pamoja na kutibiwa kwa kufanyiwa upasuaji, matibabu kwa dawa, kupata matibabu kwa njia ya eksirei yaani kuua seli za kansa.

## Maswali

1. Jina jingine la kansa ni lipi?
2. Tofauti kati ya seli za kansa na seli nyingine za mwili ni nini?
3. Uvimbe usiokuwa kansa una shida yoyote?
4. Kansa zote zina sifa zinazofanana.Thibitisha.
5. Ni kansa ipi ambayo inawapata:
   a) Kina mama.
   b) Watoto.
6. Ni vyakula vipi vinavyoweza kuchangia kushikwa na kansa?
7. Sukari ni chakula ama chanzo cha lishe ya seli za kansa. Eleza.
8. Je, kulingana na kifungu, kansa inaweza kutibiwa?
9. Orodhesha vyakula unavyopaswa kula kujikinga na kansa.
10. Orodhesha dalili za mtu kupatikana na kansa.

## Mada Ndogo 3: KUANDIKA

**INSHA**

1. Andika mazungumzo baina ya mgonjwa na daktari.
2. Umekumbana na kisa cha watu waliopata ajali ya barabarani.Andika mawasiliano yako na mhudumu wa ambulensi yakuwaokoa.

# SURA YA 6

# Mada kuu: MILA, TAMADUNI NA ITIKADI

## Mada Ndogo ya 1: Kusikiliza na kuzungumza

**Shairi**

**Soma shairi hili.**

**Tulisahau utamaduni wetu lini**
Utamaduni, utamaduni nakuita,
Swali moja mi nakuliza,
Mila zetu zilienda wapi?
Hatujiheshimu na kufurahia,
Yale mababu walituwaachia,
Wavulana masuruali yawapwaya,
Nywele nazo mitindo zimesongwa,
Wasichana uchi watembea,
Mini-sketi eti mtindo,
Chupi nadra kuvaa,
Mahaba wazi kwa yeyote,
Nalilia utamaduni wetu,

Vipofu wote tumegeuka.
Kubusiana hadharani si shida,
Lugha chafu mlo wetu,
Baba ampapasa bintiye,
Pambaja waume kwa wake mtindo,
Nauliza desturi zetu zilienda wapi?

Dini ‘mekuwa kivukio,
Misikiti kageuka soko,
Makanisa kabadilika danguroni,
Usinzi neno la wapita njia,
Hatuathiriki sisi na maovu’
Mababu kwisha sahaulika’
Waliyotunza yamepotea bure,
Nauliza desturi zetu zilienda wapi?

Baba mimba kwa ‘sichanawe si hoja,
Mimba kuavya ndiyo desturi,
Mama ‘burudishwa na mvulanawe,
Mahitaji kingono mwana amkidhia,
Jinyanya lapapasapapasa kijana,
**Unyumba limemuweka** asilani,
Nauliza jameni mila kaenda wapi?

Lugha zetu twakataa kabisa,
Kigeni ndio maongezi yetu,
Chakula cha kigeni twajibugia,
Madhara kamwe hatuyaoni,
Vinywaji vya kigeni twateremsha,
Kwa bughudha bilakujali,
Nalilia utamaduni wetu,

Nani taja kutuokoa jameni?
Ndoa haramu si kazi,
Kazi ni kuwajuvya wazazi,
Kufokea wakubwa si hoja,
Wazee kusimama magarini si hoja,
Vijana makalio twapumzisha,
Nalilia utamaduni wetu,jameni twaangamia.

Kilio kisikike nimefika tamati,
Maangamizi tumeyaona,
Naomba ya kigeni tuepuke,
Jameni turudie utamaduni wetu.

## Zoezi

1. Taja lawama za mwandishi kwa wafuataο:
    a) Kina mama
    b) Wasichana
    c) Kina nyanya
2. Taja maovu yanayotendwa na akina baba.
3. Je, dini imeathiriwaje na ukosefu wa utamaduni?
4. Kuweka mtu unyumba ni nini?
5. Kwa nini wasichana hawavai chupi?
6. Taja tabia hasi inayofanywa na wavulana.
7. Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika shairi:
    a) Yawapwaya
    b) Chupi
    c) Mahaba
    d) Bughudha
    e) Kufokea

## Kukariri shairi

**Karirianeni shairi hili.**

Uwanjani naingia, machache kuwaeleza,

Ujumbe kuwafikia, kwa makini sikiliza,
Ya muhimu zingatia, yatakufaa maisha,
Na tuepuke mila potovu, tuyanusuru maisha.

Mila potofu kataa, na hasa ukeketaji,
Watoto wadogo kuozwa, kufanya kazi za ndani,
Mizigo kutubebesha, tukosapo mahitaji,
Tuepuke mila potovu, tuyanusuru maisha.

Mwatufanyabiashara, miili yetu yanyanyaswa,
Ubakajikufanyiwa, usherati kutufanyisha,
Milapotofumwafanya,usuhuba wa lazima,
Acheni unyanyapaa,watotomtutunzeni.

Wazazi twaeleza, haki zetu tunataka,
Tupewe elimu bora, tupate malezi bora,
Mashuleni tutakwenda, kwa ibada tutakwenda,
Tuepuke mila potovu, tuyanusuru maisha.

Watoto twawaeleza, michezo baba na mama,
Vikundi vile vibaya, tusiende kujiunga,
Tutaepuka madhara, wazazi kusikiliza,
Na tuepukemila potovu, tuyanusuru maisha.

Acheni kuvichezea, vitu vyenye ncha kali,
Na sindano za mitaa, watoto tukataeni,
Mizigo kutubebesha, tukosapo mahitaji,
Na tuepuke mila potovu, tuyanusuru maisha.

Wazazi wetu twaomba, mtunusuru jamani,
Kimila twanyanyasika, upweke umetusonga,
Faraja kwetu hatuna, huruma tunaziomba,
Na tuepuke mila potovu, tuyanusuru maisha.

**Zoezi**

1. Taja mila potovu katika ubeti wa pili.
2. Kwa nini mshairi analalamika katika ubeti wa 3?
3. Taja haki mbili za watoto katika ubeti wa nne.

4. Eleza maana fiche ya maneno haya:
   a) Michezo ya baba na mama.
   b) Vitu vyenye ncha kali
   c) Sindano za mitaa

## Mada Ndogo ya 2: Kusoma

### MILA NA TAMADUNI

**Soma kisa hiki kisha ujibu maswali.**

Mila, itikadi na utamaduni ni imani, desturi na mienendo ya watu. Kila kabila huweka misingi fulani ya kitamaduni na hutambulisha watu na jamii husika.

Japo mwacha mila ni mtumwa, kuna baadhi ya mila ambazo ni potovu na zimepitwa na wakati mathalani mila zinazowadhalilisha watu fulani katika jamii na kuwanyima haki zao hususan wanawake.

Katika mila zilizopitwa na wakati ni ukeketaji wa wasichana.Waafrika walikuwa na sababu za kuwakeketa wasichana lakini kulingana na utafiti uliofanywa, madhara yake ni mengi si haba; yakiwemo kuvuja damu mpaka kufa na kuambukizwa ugonjwa wa UKIMWI kwa sababu ya kutumia kisu kimoja.

Wasichana wengi hunyimwa nafasi ya kuendelea na masomo na badala yake kuozwa kwa wanaume wasio wa rika lao na wasiowapenda. Ndoa hizi huwa za kulazimishwa hivyo mwanamke ambaye ni bibi anashurutishwa kukaa maisha ya dhiki na vitisho.

Kurithiwa kwa wajane ni desturi inayofanyika katika makabila mengi.Punde tu mume au mke wa mtu anapoaga, basi unapata kuna watu wa jamii wako tayari kumtafutia aliyeachwa wa kumwoa.Desturi hii inahatarisha maana kwanza watu hao hawaoani kwa sababu ya mapenzi bali ni shinikizo kutoka kwa jamii.Pili katika enzi hizi gonjwa la UKIMWI linafagia wengi hata wanaoonekana kuwa na afya kumbe wanameza dawa kisirisiri bila kujulikana! Utajipata umenaswa na mtego wa kifo kwa kuangalia sura ya nje tu!

Baadhi ya mila na desturi hazimtambui mtoto wa kike. Majukumu mengi na kazi za nyumbani huachiwa mtoto wa kike.Utamkuta mama akimpa mtoto wa kike kazi nyingi huku mtoto wa kiume amestarehe na pengine kutazama runinga au kulala.Wasichana wanaachiwa kazi ya kupiga deki, kufua nguo na kupika. Je, ni haki kumtenda mtoto wa kike hivi?

Makabila mengine yanashikilia sana mambo ya kuoa wake wengi.Imani ni kwamba mtu akiwa na wake zaidi ya mmoja inarahisisha majukumu ya kazi za nyumbani.Atikadiri wake wako wengi ndivyo watakavyozaana na kumpa mume hadhi! Huu ni upuuzi mtupu kwa kuwa kadiri wake na watoto wanavyokuwa, ndivyo mahitaji yanavyoongezeka.

Haya huchangia kutokidhi mahitaji ya baadhi yao.Ikumbukwe pia gonjwa la UKIMWI huletwa na kushiriki kitendo cha ndoa na wenzi wengi.Kuna hatari ya kupatwa na saratani ya sehemu za uzazi na magonjwa ya zinaa. Hata hivyo, si kila mila na utamaduni ni mbaya.Kuna mambo ya kimila ambayo ni ya muhimu kama vile kupata idhini ya wazee kabla ya kuoa, kumtambulisha mchumba wako kwa walezi wako kabla ya kuoana, kuheshimu mahali kunakochukuliwa kuwa kutakatifu na kuita mikutano ya wazee ya kusuluhisha mambo kadhaa katika jamii.Nivizuri kuzingatia mila faafu za kabila lako lakini mila zilizopitwa na wakati zitupiliwe mbali.

## Maswali

1. Eleza maana ya mila zilizopitwa na wakati.
2. Taja madhara ya kukeketa wasichana.
3. Wanawake wanaoozwa wanaume wanapata shida gani?
4. Fafanua upungufu wa kurithiwa kama mjane.
5. Ni hoja ipi inayoonyesha kudhulumiwa kwa mtoto wa kike na wazazi wake?
6. Mtoto wakiume amedekezwa vipi kulingana na kifungu?
7. Toa sababu za kupinga kuoawake wengi kulingana na kifungu.
8. Kwa nini msimulizi anasema tusiangalie sura ya nje tu?
9. Taja utamaduni mzuri kulingana na kifungu.

## METHALI

Methali hutumika kuwasilisha ujumbe maalum kwa jamii. Kuna aina mbalimbali za methali kama vile:

a) Methali za kuonya kuhusu mambo mbalimbali. Mifano;

- Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu.

c) Methali za kuhimiza ushirikiano. Mifano;

- Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu.

d) Methali za jitihada au bidii. Mifano;

- Mtaka cha mvunguni sharti ainame.

e) Methali za kuonyesha umuhimu wa undugu wa kidamu. Mifano;

- Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe.

f) Methali zinazohimiza uvumilivu. Mifano;

- Mvumilivu hula mbivu.

g) Methali zinazohimiza ustadi wa kutenda jambo. Mifano;

- Ukiona vyaelea jua vimeundwa.

h) Methali zinazotuonya juu ya tamaa. Mifano;

- Haraka haraka haina baraka.

Kulingana na maoni yako,kuna mila na tamaduni zinazopaswa kusahaulika katika jamii yako? Zitaje na ueleze kwa nini.

**KIFUNGU B**

## JAMII ZETU

**Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali.**






Makabila ya Sudan Kusini yanasifika kwa uhifadhi wa mila na utamaduni wao tangu jadi.**K**abila kubwa la Sudan kusini ni Dinka. Linajiita **Monyjaang**'.Wadinka ni kabila kubwa sana.Wao ni jumla ya watu karibu milioni 3.2. Wanachukua asilimia 25% ya idadi ya wananchi wa Sudan Kusini.

Miongoni mwa makabila yanayozingatia utamaduni wa Sudan Kusini ni kundi la Dinka,Nuer,Shilluk na Mundari ambao wanaamini kwamba wanapaswa kukatwa mistari na kuwekwa vitone vya kipekee nyusoni.Kwao,hii ni njia ya **kujitambulisha** kama kabila na urembo kwa wanawake wao.Kwa Wadinka, majukumu yamegawanywa pale ambapo wanaume hushughulikia **kunadhifisha** mashamba na wanawake kupanda, kuchota maji na kupika.

Wadinka wanathamini sana ndoa.Ndoa haivunjiki bila sababu muhimu kabisa kama mwanamke kutopata watoto.Wakati wa kipindi cha **uchumba**,mvulana hatarajiwi kushinda akimtembelea msichana pasi kuwa na marafiki wake au hata watu wa jamii yake.Kuchumbiana kunapaswa kuwa katika makazi ya msichana tu na sio kwingine.Mvulana huhitajika **kulipa mahari** ya kiwango cha juu.Wakati mwingi,mpango wa ndoa huwa wa gharama sana kwa vilekiasi cha chini cha mahari ambacho mvulana anapaswa kulipa ni ng'ombe thelathini.Haya hupangiwa na wazazi wa msichana na kwa wakati mwingi huchangiwa na tamaa ya mali na hufungwa na mila zao.

Wakati panapotokea maafa, basi huchukuliwa kama mapenzi ya Mola au kusababishwa na roho ya mtu aliyeaga.Wakati wa mazishi huchukuliwa kama wakati wa kutafuta amani na aliyeaga ili asiwadhuru.Marehemu hupewa mazishi ya heshima ili asiwe msumbufu baadaye.Mtu akifa maiti inapaswa kupelekwa msikitini siku moja baada ya kifo kutokea.Imamu husafisha na kubariki mwili wa marehemu.Maiti hufunikwa na **sanda** iitwayo 'kaftani'. Mjane na familia iliyofiwa huvaa sare nyeusi. Waislamu huamini kwamba maiti huwa na hisia hata baada ya kufa.Wanaamini kwamba viungo vya mwili havipaswi kutolewa kama msaada maana hii itasababisha marehemu asiweze kufufuka baadaye.Katika mila za kabila la Sebit Bari maiti anapaswa kuosha na kuvalishwa sare nyeupe.

Wadinka na Wanuer ni wenyeji wa Sudani ya kusini wanaojulikana kwa shughuli za uvuvi,ukulima na uwindaji.Wanafuga mifugo kwa idadi kubwa na mtu hutambulikana kutokana na idadi ya mifugo aliyonayo. Heshima na urithi wa mtu wa Wadinka hutegemea mifugo aliyonayo.Mifugo hutumika kulipia mahari.KwaWanuer idadi ya mifugo arobaini hutolewa kama mahari kwa msichana anayechumbiwa.Watoto hupewa majina kulingana na mababu zao na majina ya rangi ya mifugo waipendao zaidi.

Kabila la Wadholuo wanaoishi Sudan Kusini ni wafugaji wadogo wa ng'ombe pamoja na ufugaji mkubwa wa kondoo na mbuzi.Wengine wao ni wavuvi wanaofanya uvuvi kando ya upwa wa mito wanayoishi karibu nayo.Washilluk na Waaynuak ni wawindaji mashuhuri,nao wanawake ndio hujenga nyumba za makazi.

Kabila la Wazande kwa ujumla ni wakulima.Wao hukuza mimea mbalimbali na matunda.Kazi ya kulimani ya wanawake huku wanaume wakikinga boma.Wazande hutambulikana kwa ususi wa vikapu,meza,viti,nyuta,mishale na kofia kutoka kwa matawi na maganda ya michikicha.

Ijapokuwa makabila haya yanazingatia utamaduni kwa kina,kuna madhara yakufungwa na utamaduni huu.Kwa mfano, katika shughuli za kukatwa mistari na kuwekwa vitone nyusoni wengi huvuja damu nyingi,hutapika na kuathiri afya zao.Wakati huu wa ugonjwa wa UKIMWI, mtu anaweza kuambukizwa ugonjwa huu kwa kutumia wembe uliotumiwa na aliyeathiriwa.Mikakati ya kugharamia ndoa huchangia pakubwa katika ndoa za mapema,ukiukaji wa haki za binadamu,wanawake kuchukuliwa kama wasiojiweza na pia kulazimisha wasichana kutopata elimu.Ijapokuwa kilimo kinachangia **kukidhia mahitaji,**kwa wakati mwingi kiangazi kinapotokea,wanaume huenda malishoni mbali na familia zao kwa kipindi kirefu.Hii inaweza kusababisha kutowajibika kwa walio katika ndoa na majukumu mengi kuachiwa mwanamke.Mila,desturi na tamaduni za watu zinapaswa kuwa imani na mienendo ambayo haitamdhuru yeyote.

## Zoezi

1. Ni nini maana ya mila na utamaduni?
2. Jina Moinjaang linamaanisha nini?
3. Kwa nini makabila ya Sudan kusini yanathamini kukatwa mistari nyusoni?
4. Taja sababu moja muhimu inayoweza kuvunja ndoa katika kabila laWadinka.
5. Uchumba unathaminiwa sana Sudan Kusini. Thibitisha kwa hoja tatu.
6. Orodhesha umuhimu wa mifugo kwa wenyeji wa Sudan Kusini.
7. Taja makabila yaliyozungumziwa kwenye kifungu na shughuli wazifanyazo.
8. Fafanua majukumu ya mwanamke katika kifungu hiki.
9. Taja tamaduni tatu na ueleze madhara yake kulingana na kifungu.
10. Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika kwenye kifungu.
    a) kujitambulisha
    b) kunadhifisha
    c) uchumba
    d) kulipa mahari
    e) sanda
    f) kukidhia mahitaji

### MAPISHI YETU

**Soma kifungu kisha ujibu maswali.**





Je, wajua kwamba chakula cha kienyeji ndicho tiba ya magonjwa yote?Kwa mfano,uji ndio mlo muhimu Sudan Kusini na sio tu kama kiamsha-kinywa bali kama chakula cha kila wakati.Hutengenezwa kutoka kwa ngano,mtama,unga wa mahindi na huandaliwa pamoja na mchuzi.Mlo huu humpa mtu nguvu za utendakazi.

Kuna mlo wa maharage yaliyoviringwa kama mipira unaoitwa*tamayya.*Njugu hutumika sana ili kuongezea ladha ya chakula.Njugu huongezwa katika chakula kama nyama, mchicha na mchuzi wa njugu. Wakati mwingine njugu husagwa na kuandaliwa kama mchuzi.Mafuta ya njugu si kama yale ya kawaida yaliyotengenezewa viwandani.Haya ni mafuta yasiyo ganda kwenye mishipa, Kwa hivyo, huhakikisha afya bora.Ulaji wa njugu unasaidia sana.

*Basico* ni chakula kingine cha kienyeji cha Sudan Kusini kinachotengezwa kutoka kwa ufuta,mboga na nyama iliyokaushwa.Huandaliwa sanasana na *kabila la Kuku a*mbao ni wenyeji wa *Kajokeji.*Wao wanaamini ikiwa unataka kuwakaribisha wakwe wako,basi wapikie *Basico na Asida* na watakupenda.

Wa sudan Kusini wanasifika kwa ujuzi wa kuandaa mchuzikama *Miris* unaotengenezwa kutoka kwa mafuta ya kondoo na *okra* iliyokauka. S*harmout Abiyad* hutengenezwa kutoka kwa nyama iliyokaushwa.Pia kuna mchuzi wa *Kajaik* ambao hutengenezwa kutoka kwa samaki waliokaushwa.Michuzi hii sanasana huliwana uji wa mtama unaoitwa *Asseeda* au *Asseeda Dukun.*

Chakula ni mapishi.Je, wewe unajua jinsi ya kuandaa chakula cha kienyeji au unakimbilia tu kile utatumbukiza kwenye mafuta na usimame kando? Chakula kama tamayya huhitaji ushirikiano wa watu wengi.Jifunze kushiriki mahali ambapo kuna mapishi ili ujifunze kupika.Kumbuka jifya moja haliinjiki chungu. Usikae peke yako maana hutasoma mengi.Upishi wa chakula sampli moja unaweza kuwa na njia mbalimbali. Kwa hivyo, jifunze kutoka kwa wengine.

Ulaji wa vyakula vifaavyo ndio tiba muhimu ya magonjwa.Vyakula vyenye madini kama matunda, mboga na nafaka vinaweza kutibu magonjwa

sumbufu.Kuna sehemu za mti kama vile mizizi,matawi au hata maganda ambayo hutumika kama dawa.Mababu zetu walitumia miti hii kujiunga na kujitibu.

Matunda na mboga hutupa vitamini ambayo inatukinga dhidi ya magonjwa. Swali kuu ni je,unajivunia chakula cha kienyeji au unakimbilia vyakula ambavyo haviongezi chochote mwilini?Ni vizuri kujivunia kula vyakula vyetu vya kienyeji kuliko kujibugia vyakula visivyo na umuhimu mwilini.Tupunguze ulaji wa vyakula vyenye mafuta mengi,sukari,keki na vyakula vyote vinavyoathiri mwili wako.

## Zoezi

1. Taja aina tatu za vyakula vyenye madini.
2. Ni sehemu zipi za miti zinazoweza kutumika kama dawa?
3. Eleza umuhimu wa matunda.
4. Taja vyakula vya kienyeji vilivyotajwa kwenye kifungu.
5. Uji unatumikaje?
6. Ni chakula kipi kinachoaminika kuwanasa wageni wako?Chakula hiki kinaandaliwa na kina nani?
7. Taja aina tatu za mchuzi na jinsi ya kuandaa kila moja.
8. Msimulizi ametoa mawaidha yepi juu ya upishi?
9. Msimulizi anatuonya juu ya vyakula vipi na kwa nini?
10. Taja aina ya chakula cha kienyeji ukijuacho na uelezee jinsi ya kukiandaa.

## Mada Ndogo ya 3: Kuandika

**Resipe**

Andika njia ya kuandaa chakula cha kienyeji ukipendacho.